**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO.

**MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM)**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

# YALIYOMO


A. UTANGULIZI ........................................................................ 1

B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021 .......... 5

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ............................................ 5

D. UTEKELEZAJI HALISI KIFEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ............................................................6

E. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021 ............................................ 8

F. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022. ............................................................ 42

G. MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022 ............................................ 43

H. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ...... 44

Wizara Afisi Kuu Pemba ............................................ 53

I. SHUKRANI ............................................................ 54

J: MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022. .................. 56

VIAMBATANISHO ............................................................ 57

KIAMBATISHO NAMBA 1 A ............................................ 58

FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU ............................................ 58

KIAMBATISHO NAMBA 1B ............................................ 61

MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 ........ 61

MAPATO YANAYOINGIA HAZINA ............................................ 61

KIAMBATANISHO 1C ............................................ 61

MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA ......................... 61

KIAMBATISHO NAMBA 1D ............................................ 62

FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021
KWA KILA PROGRAMU NDOGO.................................................. 62
KIAMBATISHO NAMBA 1E...................................................... 64
FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021
KWA KILA PROGRAMU NDOGO.................................................. 64
KIAMBATISHO NAMBA 1F ...................................................... 65
BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI,
VIJANA, UTAMADUNINA MICHEZO KWA MWAKA WA
FEDHA 2021/2022.............................................................. 65
TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU .............................................. 65
TAASISI ZA RUZUKU ............................................................ 66
KIAMBATANISHO 1G............................................................ 68
BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA
2021/2022 KWA KILA PROGRAMU NDOGO ................................ 68
KIAMBATISHI NAMBA 1H ...................................................... 70
MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA
2021/2022 ......................................................................... 70
MAPATO YANAYOINGIA HAZINA............................................... 70

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO, MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima, afya njema, uwezo na nguvu za kutekeleza yale yote tuliojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile, kwa Rehema zake Mwenyezi Mungu kuibariki nchi yetu kuendelea kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufika katika Baraza hili tukiwa wazima na afya njema ili tuweze kuiwasilisha na kuijadili bajeti hii.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee na kwa dhati kabisa naomba kumpongeza **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar katika awamu ya nane kwa asilimia **76.27** na kuonesha dhamira thabiti ya kuiletea mabadiliko ya haraka nchi yetu ya Zanzibar na wananchi wake na tunamuomba Mwenyezi Mungu amlinde, ampe uzima na Afya njema ili aweze kukamilisha azma yake ya kuleta maendeleo nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kumpongeza **Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar,** kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hiyo. Hakika wananchi wa Zanzibar wana matumaini makubwa kwake na atatoa ushirikiano mkubwa katika kumsaidia vyema **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** katika majukumu yake ya kila siku ya kuleta maendeleo ya nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya kipekee naomba kumpongeza **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo ili aweze kumsaidia **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** pamoja na kuimarisha ufanisi na uwajibikaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kusimamia shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi. Ni matumaini yetu kuwa kasi itazidi zaidi kwa vile tayari umeanza vyema katika majukumu yako hayo.

6. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid,** Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa kipindi cha miaka mitano. Hii inaonesha wazi imani walioyonayo Waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini pia uwezo wako na uzoefu ulionao katika kuliongoza Baraza lako Tukufu na kuwasimamia Waheshimiwa wajumbe katika kufanikisha majukumu yao ya msingi. Kwa upande mwengine, nampongeza **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma** kwa kuchaguliwa tena katika nafasi ya **Naibu Spika wa Baraza hili.** Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shaaban Ali Othman** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Baraza hili.

7. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, naomba kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, hasa

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii **Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla** na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ya kusimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake, pamoja na kutupatia ushauri na maelekezo yaliyosaidia katika kufanikisha majukumu ya msingi ya kila siku katika Wizara yangu. Wizara yangu inafarijika sana na ushauri na maelekezo tunayopata kutoka kwa Kamati, nasema ahsanteni sana.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima natoa pole kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** pamoja na Watanzania wote kwa msiba mzito uliotokea kwa kuondokewa na alieyekuwa **Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi amin.

9. **Mheshimiwa Spika,** Pia kwa masikitiko makubwa natoa salamu za pole kwa **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kufuatia kifo cha aliyekuwa **Makamo wa Kwanza wa Rais, Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad.** Tunamuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, Amin.

10. **Mheshimiwa Spika,** dunia bado inaendelea kutafuta chanjo ya kutibu ugonjwa wa COVID-19 ambao uliibuka tena katika mwaka huu na kuweza kudhibitiwa kwa kufuata maelekezo na miongozo iliyotolewa na Serikali, wananchi wamefuata kikamilifu na kupunguza wimbi la uambukizaji wa ugonjwa huo. Nawaomba wananchi waendelee kuchukuwa tahadhari zaidi ili kuweza kujikinga na ugonjwa huo na Mwenyezi Mungu atujaalie usirejee tena katika nchi yetu. Vyombo vya Habari vya Zanzibar vilitoa mchango mkubwa sana kwa kutoa elimu kwa umma ili kujikinga na maradhi hayo.

**11. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imeundwa na sekta kuu nne ambazo ni Sekta nne za **Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo** zinazosimamiwa na taasisi 17 kama zifuatazo:-

i. Idara ya Utumishi na Uendeshaji;
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
iii. Ofisi Kuu Pemba;
iv. Idara ya Habari Maelezo;
v. Shirika la Utangazaji Zanzibar;
vi. Shirika la Magazeti ya Serikali;
vii. Tume ya Utangazaji;
viii. Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX);
ix. Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar;
x. Idara ya Maendeleo ya Vijana;
xi. Baraza la Vijana Zanzibar;
xii. Idara ya Utamaduni na Sanaa;
xiii. Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA);
xiv. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU);
xv. Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (COSOZA);
xvi. Idara ya Michezo; na
xvii. Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ).

**12. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo kwanza nitawasilisha utekelezaji wa Programu kwa mwaka wa fedha 2020/2021, uchambuzi wa mapato, matumzi pamoja na mwelekeo wa bajeti, vipaumbele na makadirio ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

## B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021

13. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na mabadiliko ya Wizara baada ya kufanyika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Wizara iliongezewa sekta ya Habari. Sekta hiyo awali ilikuwa katika Wizara inayosimamia Utalii na Mambo ya kale. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, imetekeleza Programu kuu nne nazo ni: -

i. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji;
ii. Programu ya Maendeleo ya Vijana;
iii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na
iv. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

14. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilikadiriwa kupokea **shilingi 19,406,617,670/=** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza programu kuu nne. Kati ya fedha hizo **shilingi 6,348,713,950/=** kwa kazi za kawaida na shilingi 7,157,903,720/= ni mishahara. Katika utekelezaji wa kazi za maendeleo jumla ya **shilingi 5,900,000,000/=** zilitengwa. Kati ya hizo, **shilingi 2,000,000,000/=** zilipangiwa kutekeleza Programu ya Ajira kwa Vijana, **shilingi 2,500,000,000/=** ni kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo pamoja na **shilingi 1,400,000,000/=** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya jengo la Studio za Shirika la Utangazaji Zanzibar.

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 13,233,522,375/=**. Kati ya pesa hizo, **shilingi 611,394,375/=** ni makusanyo yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, **shilingi 12,472,128,000/=** ni makusanyo yanayotumiwa na taasisi na **shilingi 150,000,000/=** ni makusanyo ya mirabaha. Idara ya Habari Maelezo ilipangiwa kukusanya **shilingi 69,111,000/=**, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) kukusanya **shilingi 224,141,000/=**, Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) **shilingi 4,000,000/=**. Pia, Tume ya Utangazaji **shilingi 314,142,375/=**, Shirika la Magazeti ya Serikali **shilingi 857,500,000/=**, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) **shilingi 1,000,000,000/=**, Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZAGPA) **shilingi 9,614,628,000/=** na Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX) **shilingi 1,000,000,000/-**.

## D. UTEKELEZAJI HALISI KIFEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, jumla ya **shilingi 7,083,573,730/=** zimepatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kazi za kawaida, sawa na asilimia **52** ya lengo la mwaka, ambapo zilikadiriwa kufikiwa **shilingi 13,506,617,670/=**. Kwa upande wa mishahara jumla ya **shilingi 5,800,335,775/=** zilipatikana sawa na asilimia **81** ya lengo la mwaka ambapo zilizokadiriwa ni **shilingi 7,157,903,720/=**. Kwa upande wa matumizi mengineyo, jumla ya **shilingi 1,283,237,955/=** zimepatikana sawa na asilimia **20** ya lengo la mwaka ambapo zilizokadiriwa ni **shilingi 6,348,713,950/=**.

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mishahara ya Idara zilizomo ndani ya Wizara, jumla ya **shilingi 2,673,715,340/=** sawa na asilimia **82** ya lengo la **shilingi 3,252,703,720/=** zimepatikana. Kwa taasisi zinazopokea ruzuku, zilipata jumla

ya **shilingi 3,126,620,435/=** ikiwa ni malipo ya mishahara sawa na asilimia **80** ya lengo la **shilingi 3,905,200,000/=**.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi mengineyo, jumla ya **shilingi 539,466,964/=** zilipatikana kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara sawa na asilimia **21** ya lengo la **shilingi 2,618,913,950/-**. Vile vile, kwa taasisi zinazopata ruzuku zilipata jumla ya **shilingi 743,770,991/=** sawa na asilimia **20** ya lengo la **shilingi 3,729,800,000/=**.

19. **Mheshimiwa Spika,** makusanyo halisi ni jumla ya **shilingi 5,510,396,502/=** sawa na asilimia **42** ya lengo la mwaka **shilingi 13,233,522,375/=**. Kwa mapato yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni Idara ya Habari Maelezo ilikusanya **shilingi 78,734,250/=**; Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) ilikusanya **shilingi 140,275,000/=**; Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) **shilingi 4,269,000/=** na Tume ya Utangazaji **shilingi 170,370,560/=**. Taasisi nyengine ambazo makusanyo yake hayaingii Mfuko Mkuu wa Serikali zikiwemo Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) **shilingi 596,891,493/=**; Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP) **shilingi 2,880,754,708/=**; Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX) **shilingi 958,548,262/=**; Shirika la Magazeti ya Serikali **shilingi 592,990,940/=**. Vile vile, **shilingi 87,562,289/=** sawa na asilimia **58** ikilinganishwa na lengo la **shilingi 150,000,000/-**. Fedha hizi ni makusanyo ya mirabaha ya wasanii na wabunifu yanayokusanywa na Afisi ya Hakimiliki (COSOZA).

20. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za maendeleo zinazotokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, **shilingi 1,831,579,010/=** zimepatikana sawa na asilimia **31** ya lengo la mwaka **shilingi 5,900,000,000/=**.

21. **Mheshimiwa Spika,** Mpaka Machi 2021, Wizara imeshatumia **shilingi 1,231,579,010/=** kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo ambapo sawa na asilimia **49** ya lengo la mwaka **shilingi 2,500,000,000/=**.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika Programu ya Ajira kwa Vijana, Wizara imeshatumia jumla ya **shilingi 600,000,000/=** sawa na asilimia **30** ya **shilingi 2,000,000,000/=**.

23. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Studio ya Mkanjuni **shilingi 1,147,696,900/=** zimepatikana kwa ajili ya ujenzi huo. Aidha, katika Mradi wa Ununuzi wa vifaa vya Studio na samani za studio hadi kufikia Machi, 2021 fedha hizo hazikupatikana.

24. **Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa fedha zilizopangwa kwa mwaka 2020/2021 na zilizopatikana hadi kufikia Machi 2021 umeainishwa katika **Kiambatanisho Namba 1A-1C**

## E. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021

### i. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji

25. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inaundwa na programu ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji.

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 8,458,062,270/=**, kati ya hizo **shilingi 4,039,678,820/=** ni mishahara na **shilingi 3,018,383,450/=** ni matumizi mengineyo. **shilingi 1,400,000,000/=** kwa ajili ya Mradi wa Ununuzi wa vifaa vya studio Pemba. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 3,933,508,108/=** sawa na asilimia **47** zilipatikana kati ya hizo **shilingi 2,913,018,261/=** ni mishahara na **shilingi 1,020,489,847/=** ni matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo 1: Upatikanaji na Usambazaji wa Habari**

27. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari inatekelezwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS), na Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX). Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 5,765,762,270/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 3,031,014,502/=** sawa na asilimia **53** zilipatikana **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba1D**)

28. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programu ndogo hii ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari, Shirika la Utangazaji Zanzibar limefanikiwa kurusha jumla ya vipindi **8,753** vya Televisheni na vipindi **14,028** vya Radio vya ndani na nje vinavyohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa Unguja na Pemba, maadhimisho ya miaka **57** ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi pamoja na vipindi vya burudani, Michezo na vipindi vya kawaida. Jumla ya matangazo **16,731** yamerushwa hewani kupitia Redio na TV yakiwemo matangazo ya vifo, biashara na matangazo maalumu. Kati ya vipindi hivyo **1,139** ni kutoka Pemba. Hali hii imepelekea wananchi wengi kupata habari za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira ambazo zimewasaidia kuelimika, kupata burudani na kufanya maamuzi mbali mbali.

29. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeweza kurusha matangazo ya moja kwa moja **159** ambayo ni ya kitaifa na shughuli za Viongozi wakuu wa Serikali ikiwemo Maziko ya aliyekuwa **Makamo wa Kwanza wa Rais Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad** na kuuaga mwili wa aliyekuwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli.** Pia, matukio mengi ya Serikali yakiwemo yale yanayomuhusu **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na**

**Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** yamerushwa hewani moja kwa moja na kuwapa taarifa sahihi na kwa wakati wananchi wa mjini na vijijini. Inakadiriwa zaidi ya watu **4,000,000** wamepata habari za kijamii, kisiasa na kichumi ndani na nje ya Zanzibar. Wakati wa mripuko wa maradhi ya Korona, ZBC kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali ilirusha maudhui ya elimu na kuwapa elimu watoto wetu wakiwa nyumbani. Matokeo ya kurusha matangazo haya ni kuwafanya wanafunzi kusoma wakiwa nyumbani na kuweza kufaulu katika mitihani yao ya Taifa ya darasa la nne, la sita, la kumi na la kumi na mbili.

30. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa habari juu ya kudorora kwa uendeshji wa ZBC, Wizara iliunda Kamati maalum ya Uchunguzi wa Shirika hilo. Ripoti ya Kamati hiyo iliwasilishwa Wizarani na pia kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Napenda kulijulisha Baraza lako tukufu kwamba Serikali imechukua hatua kupitia mapendekezo ya ripoti hiyo ili kuliimarisha Shirika na kuleta utendaji bora. Bodi ya ZBC ilivunjwa na kuundwa Bodi mpya. Sasa nidhamu na ufanisi wa kazi umeongezeka na ni imani yetu kwamba chombo hiki muhimu kitafanya kazi kwa weledi mkubwa na kufuata maadili ya habari.

31. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kusambaza taarifa **675** za kiuchumi, kisiasa na utamaduni zikiwemo harakati za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ufunguzi wa Miradi ya maendeleo, Kongamano la nne la Kimataifa la Kiswahili. Taarifa hizi ziliandikwa na kusambazwa kwenye vituo mbali mbali vya habari kama vile ZBC Redio, ZBC TV, Chuchu FM Redio, Redio Istiqama pamoja na redio za jamii Micheweni na Tumbatu. Aidha taarifa ziliwekwa kwenye bango la kielektroniki ***(Display Board)*** lililopo Kisonge na kuweka taarifa kwenye mitandao ya kijamii ili wananchi walio wengi kupata taarifa zinazotokea kwenye

nchi na kwa wakati. Vile vile, Idara imeweza kutoa taarifa maalumu ***(Press releases)*** kwa vyombo vya habari na umma. Taarifa hizo zilikua na maudhui mbali mbali ikiwemo uteuzi wa viongozi mbali mbali wa Serikali kitaifa. Hali ambayo inaisidia jamii kuelewa matukio ya nchi yao.

32. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeweza kusambaza jumla ya picha za Viongozi Wakuu wa nchi zikiwemo picha **2,131** za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, picha **220** za Hayati Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na picha **173** za Rais Wastaafu. Pia, Idara ilitoa vibali vya kupiga picha za kutengenezea filamu zitakazopelekea kuongeza mapato ya Serikali kupitia mfuko Mkuu wa Hazina na pia kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kudhibiti, kusimamia na kuwawezesha Waandishi wa Habari waliopo nchini kufanya kazi zao bila vikwazo, Idara imetoa vitambulisho **175** vya Waandishi wa Habari kwa lengo la kusaidia kusimamia weledi wa waandishi na kutopotosha umma kupitia tasnia ya habari na mawasiliano.

34. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) limefanikiwa kuchapisha magazeti ya ***Zanzibar Leo, Zanzibar Leo Jumapili, Zaspoti, Zanzibar Mail na Zanzibar Leo Wanawake*** na kuyasambaza katika Mikoa yote ya Tanzania kwa lengo la kutoa habari, kuburudisha na kuelimisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Shirika limefanikiwa kuchapisha jumla ya nakala **451,750** kwa magazeti yote yanayochapishwa kila siku, wiki na kila mwezi. Pia Shirika limefanikiwa kutoa matangazo **855** kwa Unguja na Pemba katika magazeti yake na kuongeza kiwango cha mapato.

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka ujao wa fedha 2021/2022 Shirika linakusudia kuongeza wigo wa uchapaji na usambazaji wa magazeti kwa kuchapisha jumla ya nakala **10,000** kwa gazeti la kila siku na nakala **3,000** za magazeti ya kila wiki na kila mwezi ambayo yanatarajiwa kuchapwa na kusambazwa katika Mikoa ya Tanzania.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kuongeza wigo wa usambazaji wa magazeti na kuongeza idadi ya wasomaji, Shirika limefungua ofisi yake mpya Dodoma ambayo itasaidia kuongeza soko zaidi kupitia Taasisi za Serikali na binafsi zilizopo Dodoma na maeneo ya jirani kwa ununuzi wa magazeti na pia kwa ajili ya kupata matangazo mbali mbali.

37. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMX) imefanikiwa kuuza ving'amuzi **21,451** kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Kampuni imefanikiwa kuleta ving'amuzi **11,000** na antena **9,600**. Kampuni inategemea kupata idadi kubwa ya wateja hadi kufikia **32,451** mwishoni mwa mwaka 2021. Aidha, Kampuni imenunua kifaa kipya cha **ELECTRA XT** kwa ajili ya kuipa mitambo uwezo wa kuongeza chaneli nyingi zaidi.

38. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni katika kuhakikisha maudhui yanapatikana muda wote bila kukosekana, imefanya ufuatiliaji katika vituo vyake vyote saba vya Unguja na Pemba na kuvipatia huduma ya umeme na mafuta. Vituo hivyo ni Masingini, Rahaleo, Nungwi na Muyuni kwa Unguja na Bungala, Kichunjuu na Chake Chake kwa Pemba. Vile vile, Kituo cha Masingini kimepatiwa jenereta jipya la KVA 35 ambalo litasaidia kuendelea na kazi iwapo umeme utazimika.

39. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni hii kwa miaka mitatu mfululizo, imeweza kuendesha biashara. Kumekuwa na ongezeko la makusanyo kila mwaka. Mpaka kufikia Machi 2021, jumla

ya **shilingi 958,548,262/=** zimekusanywa sawa na asilimia **64** na matarajio ni kukusanya **shilingi 1,500,000,000/=** kufikia June 2021.

***Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Studio za ZBC Pemba***

**40. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Studio za ZBC Pemba unatekelezwa katika programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu ya tatu ambapo kwa mwaka 2020/2021 umepatiwa jumla ya **Shilingi 1,147,696,900/=** sawa na asilimia **64** hadi kufikia Machi, 2021.

**41. Mheshimiwa Spika,** Ujenzi huu wa Ofisi na Studio za ZBC unatekelezwa na CHUO CHA MAFUNZO na sasa upo katika hatua za kumalizika ambapo tayari jengo la ghorofa tatu pamoja na kuezekwa limemalizika. Aidha utiaji wa Plasta ya ndani na nje, milango ya chuma na madirisha, pamoja na miundo mbinu ya umeme na maji vikiwemo vyoo na matangi ya maji tayari yamewekwa. Hivi sasa kazi ya utiaji tiles na milango inaendelea. Wastani wa kazi iliyofanyika inakaribia asilimia **80**.

**42. Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kuwa mradi huu ulianzia katika Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale na tayari wamekabidhi nyaraka mbali mbali kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na pia kumtambulisha Mkandarasi. Hata hivyo Uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliviomba vyombo vya uchunguzi (ZAECA) kufanya ukaguzi ili kujiridhisha kama jengo limekidhi matakwa ya kimkataba na linalingana na thamani ya pesa zilizolipwa. Hadi sasa Wizara haijapokea taarifa rasmi kutoka kwa vyombo vya uchunguzi.

**43. Mheshimiwa Spika,** Uongozi wa Wizara umeshafanya ziara ya kwenda kulitembelea jengo hilo na kuona kasoro zilizopo

na pia viongozi mbali mbali wa Serikali wamefika kuangalia utekelezaji wa mradi wa ujenzi huo wakiwemo wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa jamii na uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

***Mradi Wa Ununuzi Wa Vifaa Vya Studio, Samani Za Ofisi, Vifaa Vya Kompyuta na UPS (Uncorrupted Power Supply)***

44. **Mheshimiwa Spika,** mradi wa ununuzi wa Vifaa vya Studio, Samani za Ofisi, vifaa vya kompyuta na UPS unatekelezwa katika programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari. Kwa mwaka 2020/2021 mradi huo ulipangiwa jumla ya **shilingi 1,400,000,000/=** hadi kufikia Machi, 2021 mradi huu haukuingiziwa fedha.

45. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umeshakamilisha taratibu za manunuzi na kinachosubiriwa ni kuingiziwa fedha tu kutoka serikalini ili wizara iweze kuendelea na taratibu za manunuzi.

***Programu Ndogo 2: Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji***

46. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,033,762,270/=**. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 1,377,392,013/=** sawa na asilimia **68** zilipatikana. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D)**

48. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutoa vibali kwa vyombo vya habari 21 vikiwemo ELEPHANT

AFRICA, DEEMAX TV, TBS News, ZDF German TV vya uchukuaji wa picha na filamu katika maeneo mbalimbali kwa kutengenezea filamu na Makala. Matokeo ya kutoa vibali hivyo ni kuongeza mapato kwa Serikali.

49. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utangazaji imefanikiwa kutoa jumla ya leseni **16** za vituo vya utangazaji vikiwemo redio **4,** televisheni **2** na maudhui ya mitandaoni 10. Kati ya hizo **4** za redio ni Swahiba FM, Chuchu FM, Adhana FM na Maria FM. Leseni mbili za Televisheni nazo ni Top Plus TV na Annour Africa TV. Leseni 10 za TV za mitandaoni zikiwemo HIKS Media online, ZSSF online, Zanzibar Yetu online, Jozani online, RVS online, JAI online, ZAGPA online, na Green Waves online. Aidha, Tume imefanikiwa kufuatilia na kurekodi matangazo ya vituo **23** vya redio za FM na vituo **28** vya Televisheni za mitandaoni vikiwemo Coconut FM, Zenj FM, Spice FM, Alnour FM na Swahiba FM.

50. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha maadili ya utangazaji hayakiukwi, Tume ya Utangazaji Zanzibar imetafsiri Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar ya mwaka 1997 na imeshapelekwa Baraza la Kiswahili kwa ajili ya kufanyiwa uhariri. Aidha, Tume ya Utangazaji Zanzibar imefanya mikutano minne na wadau wa utangazaji nchini. Mikutano hiyo inahusu ulipaji wa ada za leseni na kufuata maadili ya utangazaji, kufuata muongozo wa huduma za utangazaji wakati wa Uchaguzi Mkuu, pamoja na kujadili mikakati ya kuiendeleza tasnia ya Utangazaji. Matokeo ya mikutano hiyo ni kuwa kumekuwa na ongezeko la kulipa ada na pia kufuata kanuni za utangazaji. Tume ilichukua hatua kwa mujibu wa kanuni kwa vituo vilivyo kwenda kinyume na maadili na kuwapa onyo baadhi ya vyombo vya habari.

51. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na kupata ufanisi, Tume ya Utangazaji Zanzibar imefanikiwa kuipatia ofisi vifaa vya kuandikia, huduma za

umeme na kulipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo likizo na muda wa ziada kwa lengo la kupatikana ufanisi zaidi katika kazi.

52. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar imefanikiwa kuchapisha nyaraka na taarifa **336** za Serikali Kuu zinazowasilishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nyaraka hizo ni pamoja na Miswada, Kanuni, Sheria na Magazeti Rasmi ya Serikali. Aidha, Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar imepokea jumla ya kazi **786** za uchapaji zenye thamani ya **shilingi 2,512,626,829/=**. Kati ya hizo, kazi **743** zimekamilika na kazi **43** zinaendelea kuchapishwa. Pia, kati ya kazi hizo, **663** kutoka katika Taasisi za Serikali na **123** za taasisi binafsi.

53. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar pia imechapisha jumla ya nakala **451,750** za Magazeti yanayosambazwa na Shirika la Magazeti la Serikali. Uchapishaji huu wa Magazeti ni kazi ambayo hufanyika kila siku.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar inaendelea na jukumu lake la kila siku la kuimarisha mitambo yake ya uchapaji. Jumla ya mitambo **12** imefanyiwa matengenezo madogo na mitambo **4** imefanyiwa matengenezo makubwa. Pia, mtambo wa uchapishaji wa madaftari umekamilika na mtambo huo tayari umeshafungwa katika eneo la kiwanda cha uchapaji.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisi na kuandikia, Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar imepokea maombi ya huduma kutoka katika Taasisi **36** na Taasisi zote zimepatiwa huduma kwa vifaa vilivyokuwepo. Wakala inatafuta maghala ya kuweka vifaa vyake hasa vile vya kiofisi ili kuimarisha ufanisi wa kazi zake.

### ii. Programu ya Maendeleo ya Vijana

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,521,115,000/=**, kati ya fedha hizo, **shilingi 148,915,000/=** ni mishahara na **shilingi 372,200,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa ajili ya Programu ya Ajira kwa Vijana. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya **shilingi 801,673,00/=** zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia **32** ya makadirio kati ya hizo **shilingi 111,883,020/=** ni mishahara na **shilingi 89,790,000/=** ni matumizi mengineyo na **shilingi 600,000,000/=** kwa ajili ya Programu ya Ajira kwa vijana

***Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana***

57. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Baraza la Vijana Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo hii iliidhinishiwa **shilingi 372,200,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 89,790,000/=** sawa na asilimia **24** zilipatikana ***(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D).***

58. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa programu ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Idara ilipanga kutekeleza shughuli ya maadhimisho ya siku vijana Kimataifa; kutembelea vikundi vya kiuchumi vya vijana pamoja na kushajiisha vijana waliomaliza vyuo vikuu kuanzisha vikundi vya kiuchumi; kuwezesha na kufuatilia shughuli za maendeleo ya kiuchumi za vijana. Vile vile, kuandaa mabonanza ya michezo kuhamasisha upimaji wa VVU, elimu ya afya ya uzazi, kupima afya na kujiunga na U-Report kwa vijana chini ya udhamini wa UNICEF na UNFPA. Pia, kuyajengea uwezo na uzalendo mabaraza ya Vijana ya Wilaya na vijana kwa ujumla ili kuongeza ari ya kujitolea pamoja na kuratibu mbio za mwenge wa Uhuru.

59. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanikiwa kuandaa kongamano la siku ya Vijana na siku ya kujitolea Kimataifa ambapo jumla ya vijana 1,100 walishiriki kutoka Unguja na Pemba wakiwemo vijana kutoka mabaraza ya vijana ya Wilaya zote, taasisi mbali mbali za vijana, wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za Serikali wakiwemo vijana wa Mabaraza ya Vijana. Ujumbe kwa mwaka 2020 katika kongamano hilo ulikuwa ni "Kijana Shiriki Uchaguzi, Dumisha Amani".

60. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya ufuatiliaji kwa vikundi vya kiuchumi vya vijana **97** (Unguja 50 na Pemba 47) kwa lengo la kujua maendeleo ya shughuli zao, mafanikio, changamoto na kuwapatia ushauri wa kitaalamu. Aidha, vikundi viwili vya kiuchumi vya vijana vimewezeshwa kwa kupatiwa msaada wa vifaa vya ushoni na pembejeo za kilimo. Vikundi hivyo ni Baraza la Vijana Shehia ya Mtofaani Wilaya ya Magharibi ''A" na Kikundi cha Wahitimu PDS, Tunguu Wilaya ya Kati.

61. **Mheshimiwa Spika,** katika kuyajengea uwezo na uzalendo mabaraza ya Vijana ya Wilaya na vijana kwa ujumla imefanikiwa kufanya uchaguzi wa Baraza la Vijana Zanzibar kuanzia ngazi ya Shehia na Wilaya ambapo Shehia zote **388**, Wilaya **11** na Taifa kwa Unguja na Pemba zimekamilika. Kwa ujumla, uchaguzi umeenda salama. Tume huru ya Uchaguzi ilifanya kazi nzuri na kwa weledi mkubwa.

62. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kuhamasisha Vijana mbali mbali kujiunga na Baraza la Vijana ambapo Vijana wengi wamehamasika na wamejitokeza kuchukua fomu katika Shehia zao na kufanya idadi ya Wanachama wa Baraza la Vijana Zanzibar kuongezeka kutoka **17,540** na kufikia **18,833** wakiwemo wanaume **9,214** na wanawake **9,619** ni sawa na ongezeko la wanachama **1,293.** Baraza linatarajia kuongeza wanachama zaidi kwa mwaka fedha 2021/2022.

63. **Mheshimiwa Spika,** katika mikakati ya kuwawezesha vijana kujiajiri, Baraza limeweza kufanikisha makongamano **2** ya kuibua fursa za ajira kwa vijana wahitimu wa Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini Unguja. Jumla ya vijana **100** (wanawake 51 na wanaume 49) walishiriki. Fursa zilizoibuliwa ni kuanzisha kampuni ya utoaji wa huduma za mahitaji mahotelini, masoko kwa wazalishaji wadogo wadogo, usindikaji wa mananasi, kilimo cha kisasa na kusindika ndimu na mapesheni, ufugaji na kilimo cha mboga mboga na matunda. Hali hii imewasaidia vijana kupata mwanga wa kujiajiri na kujiongezea kipato.

64. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Maendeleo ya Vijana imezindua Mpango Mkakati wa Ushirikishwaji wa Vijana wenye lengo la kuwashirikisha vijana katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mpango huu umeainisha maeneo saba ya kimkakati katika kuwashirikisha vijana na kuwawezesha ikiwa ni pamoja na Elimu, Kilimo, Ajira, Afya, Mazingira na mabadiliko ya Tabia nchi, ushiriki wa kisiasa na Maisha ya Jamii. Mkakati huu umekamilika na tayari umeshazinduliwa na jumla ya vijana **130** (72 wanawake na 58 wanaume) walishiriki kutoka taasisi za Serikali, taasisi binafsi na vijana kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba na kupatiwa nakala za Mkakati huo kwa ajili ya Utekelezaji.

65. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, vijana **138** wakiwemo (wanawake 102 na wanaume 36) walishiriki katika mafunzo ya afya ya uzazi na uongozi wakiwemo vijana wa mabaraza ya vijana, vijana wa vyuo vikuu pamoja na vijana waliotoka katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Jumla ya vipindi **33** kupitia redio vilirushwa ambapo mada **11** za muongozo wa stadi za maisha zilirushwa hewani kupitia vyombo vya habari ili kuwafikia vijana walio wengi. Faida ya kushiriki mafunzo hayo ni kwa vijana kujielewa zaidi na kupata taaluma inayowasaidia kujitambua na kufanya maamuzi sahihi katika afya ya uzazi.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa makala *(documentary)* ya vijana wa kike wa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Kwa Unguja vijana **21,** na Pemba vijana **12** (vijana watatu kwa kila Wilaya) walioshiriki katika utengenezaji wa Makala ambao ni miongoni mwa waliogombea nafasi mbali mbali za uongozi kwa uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Makala imekamilika na itatumika kama ni nyenzo ya kushajiisha vijana wengine wa kike kugombea nafasi mbalimbali za Uongozi.

67. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu inaratibu mbio za Mwenge wa Uhuru. Kwa mwaka 2021, uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru umefanyika tarehe 17 Mei 2021 katika Uwanja wa Mwehe, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja. Ujumbe wa mwaka huu ni **"Tehama ni Msingi wa Taifa Endelevu: Itumie kwa Usahihi na Uwajibikaji".** Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika mbio za Mwenge mwaka huu. Shukran maalum ziende kwa Ofisi ya Rais, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Wizara ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Wilaya na Mikoa kwa maandalizi na utekelezaji wa mbio za Mwenge wa Uhuru.

**Programu ya Ajira kwa Vijana**

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ajira kwa Vijana inatekelezwa ndani ya programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Programu ya Ajira kwa Vijana imepangiwa kupatiwa **shilingi 2,000,000,000/=** hadi kufikia Machi 2021 programu hii imepatiwa **shilingi 600,000,000/=** sawa na asilimia **30.** Fedha hizi zimetumika kwa ununuzi wa Boti **6** na ununuzi wa vifaa vya vijana waliosomea uchongaji na uchomaji.

**69. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 programu ya Ajira kwa Vijana ilipangiwa kuwasaidia vijana katika shughuli za kiuchumi zikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, kuwapatia mafunzo kazi, kuwapatia vifaa vya kufanyia kazi pamoja na uibuaji wa vipaji vya michezo. Jumla ya vijana **383** wamenufaika katika programu hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021

**70. Mheshimiwa Spika,** katika kuwasaidia vijana katika shughuli za kiuchumi, Wizara imenunua boti **6** aina ya faiba pamoja na nyavu seti **5** na mashine **6** aina ya Yamaha (horse power15) kwa ajili ya kuwaendeleza vijana katika fani ya uvuvi ili kuweza kujiendeleza katika shughuli za uvuvi ambapo jumla ya vijana **137** wamenufaika katika mgao wa boti hizo.

**71. Mheshimiwa Spika,** Boti hizo zimetolewa kwa vijana wa Mabaraza ya Vijana ya Shehia za Unguja na Pemba. Mabaraza yaliyopatiwa boti hizo ni Baraza la Vijana Shehia ya Mtoni (Magharibi A), Baraza la Vijana Shehia ya Ng'ambwa (Kati), Baraza la Vijana Shehia ya Sizini (Micheweni), Baraza la Vijana Shehia ya Shungi (Chake Chake), Baraza la Vijana Shehia ya Tasini , na Baraza la Vijana Shehia ya Nungwi (Kaskazini A). Baadhi ya vijana wameanza kupata gawio kutokana na kazi za uvuvu na shughuli za baharini.

**72. Mheshimiwa Spika,** katika kuwaendeleza vijana ili kuweza kujiajiri wenyewe na kupunguza wimbi kubwa la ukosefu wa ajira za Serikali, Wizara imefanikiwa kununua vifaa vya kuchongea na kuchomea kwa ajili ya vijana **246** Unguja na Pemba ambao walipatiwa mafunzo ya miezi **6** ya uchongaji na uchomaji vyuma kupitia programu ya Ajira kwa Vijana katika vyuo vya Amali Mkokotoni, Vitongoji na Chuo cha Polisi Ziwani. Tunaushukuru uongozi wa Equity Bank kwa kutoa mafunzo ya udhibiti wa fedha, bajeti na mikopo bila ya malipo kwa vijana hao waliomaliza mafunzo haya kwa

upande wa Unguja na sasa wanajiandaa kutoa mafunzo hayo kwa upande wa Pemba.

73. **Mheshimiwa Spika,** Vijana hao ambao wamepatiwa mafunzo tayari vifaa vyao vilitolewa kwa waliosomea ushoni kwa hatua ya awali na vile vya uchomaji na uchongaji tayari vishakabidhiwa kwa wakuu wa wilaya kwa ajili ya kuwapatia vijana na kwa usimamizi . Aidha kwa upande wa Pemba vifaa hivyo vimeshakabidhiwa kwa Afisa Mdhamini kwa ajili ya kuwakabidhi Wakuu wa Wilaya.

**iii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.**

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 5,887,148,000/=**. Kati ya hizo, **shilingi 1,578,748,000/=** ni mishahara na **shilingi 1,808,400,000/=** ni matumizi mengineyo, na **shilingi 2,500,000,000/=** kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 2,914,616,920/=** sawa na asilimia **50** zilipatikana. Kati ya hizo **shilingi 1,389,058,910/=** ni mishahara, **shilingi 293,979,000/=** ni matumizi mengineyo na **shilingi 1,231,579,010/=** ni mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.

75. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inaundwa na programu ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo.

**Programu Ndogo 1: Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa .**

76. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inaundwa na Idara ya Utamaduni na Sanaa, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu

na Utamaduni, (BASSFU), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (COSOZA).

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, programu hii ndogo iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,609,948,000/=** kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa mapato, ilikadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi 378,141,000/=**. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 1,618,421,910/=** sawa na asilimia 62 zilizopatikana na kufanikiwa kukusanywa jumla ya **shilingi 232,106,289/=** sawa na asilimia **61** (**angalia Kiambatanisho namba.1D).**

78. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza na kuendeleza utamaduni, Wizara imefanikiwa kuandaa Tamasha la 25 la Utamaduni wa Mzanzibari kwa Unguja na Pemba. Tamasha hili limeweza kuonesha sanaa mbali mbali za kiutamaduni, maonesho ya bidhaa na kazi za kiutamaduni, mavazi ya kiasili ya Kizanzibari, maonesho ya vyakula vya Kizanzibari na burudani kupitia ngoma za asili kutoka katika Wilaya za Unguja na Pemba pamoja na maonesho ya fensi.

79. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na jitihada za kuhifadhi na kufufua kazi za Sanaa na utamaduni wa Mzanzibari. Kwa kupitia programu hii, imeanza kuainisha aina za ngoma zinazopatikana katika maeneo ya kisiwa cha Pemba kwa kuanzia na maeneo ya Kangagani na Wesha. Lengo ni kuzifufua na kuziendeleza ngoma hizo zilizoanza kutoweka ili kuweza kuendelea kutumika.

80. **Mheshimiwa Spika,** elimu juu ya umuhimu wa kazi za Sanaa na utamaduni imetolewa kupitia kipindi cha *"Mswahili na Utamaduni"* kinachorushwa kupitia ZBC Radio. Jumla ya vipindi vinane (8) vimerushwa na inakadiriwa zaidi ya wasikilizaji **800,000** wamefikiwa. Matokeo ya taaluma hii ni kuwaandaa wananchi kujua mila na desturi zao na kuzienzi. Vile vile, mafunzo kwa vijana walioachana na madawa ya

kulevya yalitolewa kupitia maigizo na filamu ili waweze kujiendeleza na kuachana na mambo maovu. Matokeo yake ni kuitumia sanaa kuwabadilisha vijana kuwa raia wema ambao wanajishughulisha na harakati za kiuchumi na hivyo kuongeza ajira na kipato kwa vijana.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza shughuli za Sanaa na wasanii, Wizara imeimarisha Studio ya Filamu kwa kuiunganisha na mkonga wa mawasiliano wa Taifa ili kuboresha huduma na kurahisisha utoaji wa huduma katika studio kuwa na kasi zaidi. Studio hiyo ambayo inatumika katika kurikodi kazi za wasanii mbalimbali imefanikiwa kurikodi kazi tatu 3 ikiwemo kazi za filamu mbili na kazi moja ya muziki.

82. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kukutana na wazee walioshiriki katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika kwa kupata taarifa za ushiriki wao katika ukombozi wa Bara la Afrika na maeneo yaliyotumika katika harakati hizo. Lengo lake ni kukusanya taarifa zinazohusiana na ukombozi wa Bara la Afrika na kuweka kumbukumbu za maeneo hayo kwa ajili ya kuhifadhi na kuweka kielelezo cha utamaduni wa Afrika.

83. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa maazimio ya vikao vya Ushirikiano kati ya SMT na SMZ kupitia BAKIZA na BAKITA kwa mara ya kwanza, Wizara imeadhimisha siku ya Kiswahili kwa kuwasilisha makala mbali mbali zikiwemo Kiswahili na Uchumi wa Buluu; Uchunguzi wa Fursa na Changamoto za Ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kama bidhaa nchini Tanzania na kumbukizi ya marehemu Muhamed Said Abdulla. Mwaka wa 2020/2021 maadhimisho ya siku ya Kiswahili yamefanyika Tanzania Bara katika mkoa wa Dodoma. Kwa mwaka wa fedha unaokuja wa 2021/2022 maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika Zanzibar katika kisiwa cha Pemba.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza Kiswahili, Wizara imefanikiwa kuandaa kongamano la nne la Kiswahili la Kimataifa lililowashirikisha wataalamu, wadau na wapenzi wa Kiswahili ndani na nje ya nchi. Washiriki 236 kutoka nchi tofauti ikiwemo Tanzania Bara, Marekani, Kenya, Burundi na wenyeji Zanzibar walipata fursa ya kujadili mada mbalimbali ikiwemo mada ya Kuchangamkia Fursa za Soko la Kiswahili Duniani.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza Kiswahili, Baraza la Kiswahili Zanzibar limezindua kitabu cha Dk. Shein na Maendeleo ya Kiswahili Zanzibar 2010-2020 na nukuu za Dokta Shein katika Maendeleo ya Kiswahili. Aidha, maneno **36** ya vipeperushi vya msamiati (Kamusini Leo) yamerushwa katika mitandao ya kijamii. Hali ambayo imepelekea wananchi maana halisi ya msamiati na hivyo kupunguza kupotosha lugha ya Kiswahili.

86. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kukisimamia Kiswahili kuwa bidhaa yenye kuleta tija, nchi imeendelea kutangaza machapisho ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar ambapo jumla ya machapisho **17** yameuzwa likiwemo kamusi la Kiswahili Fasaha, Kamusi la lahaja ya Kitumbatu, Kamusi la lahaja ya Kipemba, Kamusi la lahaja ya Kimakunduchi, Jarida maalumu la Kongamano, Kitabu cha Mawasiliano ya Msingi ya Kiswahili kwa Wageni, kitabu cha Utamaduni wa Mzanzibari na kitabu cha Dkt. Shein na Maendeleo ya Kiswahili.

87. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuimarisha na kuendeleza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar, jumla ya vipindi 74 vya Kiswahili vimetayarishwa na kurushwa kupitia vyombo vya habari vikiwemo ZBC TV, AZAM TV, ITV, ZCTV na redio, TBC, Habari FM, Coconut FM, Redio One, Redio jamii Micheweni, UFM, Rubondo FM, Sauti ya Ujerumani, Hits FM, Mwenge FM, Istiqama FM, Asalam FM na Chuchu FM.

**88. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuhakikisha inasimamia maadili ya kizanzibari yasipotee na kuwa na sanaa yenye kuonesha maadili yaliyo mema pamoja na udhibiti wa kazi za sanaa, imefanikiwa kukagua kazi za sanaa za monesho **265** zikiwemo sanaa za maonesho ya jukwaani **50,** kazi hizo zimefanyiwa ukaguzi kwa kuzifanyia uhakiki wa kutolewa makosa ya kisanaa na maelekezo ya maadili ili ziweze kutumika hadharani. Aidha vikundi **63** vya Sanaa na Utamaduni Unguja na Pemba vimesajiliwa upya kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa mujibu ya sheria ya BASSFU namba **7** ya mwaka 2015.

**89. Mheshimiwa Spika,** jumla ya kazi za Hakimiliki **646,** sawa na asilimia **185** ya makadirio ya Usajili zimesajiliwa katika mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuhifadhi na kupata takwimu halisi za kazi za wasanii zilizosajiliwa. Miongoni mwa kazi hizo ni kazi **239** za Muziki wa Kizazi kipya, kazi **218** za Kasida, kazi **25** za muziki wa taarab, muziki wa Jazz kazi **7,** muziki wa Injili kazi **65,** Filamu **51,** Vitabu **18,** Makala fupi **5,** michoro na picha **3,** programu **14** na mawaidha **1.** Wasanii wengi wamehamasika kusajili kazi zao kutokana na jitihada zinazochukuliwa na Wizara kupitia Afisi ya Hakimiliki za kupambana na uharamia, hivyo kuwa na imani ya kupata usimamizi mzuri wa haki zao.

**90. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ofisi ya Hakimiliki hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kukusanya Mirabaha yenye thamani ya **shilingi 87,562,289/=** sawa na asilimia **58.** Mirabaha hiyo imekusanywa kutoka kwa watumiaji mbalimbali wa kazi za Hakimiliki kibiashara, wakiwemo wenye mahoteli, kumbi za burudani, viwanja vya kufurahishia watoto na maduka ya kuuza na kukodisha vinasa sauti na picha. Fedha hizo zitagaiwa kwa wasanii na wabunifu wapatao **1,300** wa vikundi mbalimbali vya sanaa na ubunifu vikiwemo vikundi vya Taarab, Muziki wa kizazi kipya, Muziki wa Injili, Kasida, filamu, Maigizo na Mawaidha.

**91. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Hakimiliki imefanikiwa kuanza kutumia kanuni ya usimamizi wa kazi za maandishi ya mwaka 2019 ambapo inaendelea kufanya mazungumzo na watumiaji wa kazi za maandishi kibiashara kwa kuwataka wafanye malipo ya matumizi ya kazi za Hakimiliki, zikiwemo taasisi za elimu za umma na binafsi na wenye maduka ya kutoa fotokopi.

**92. Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukuwe nafasi hii, kuipongeza Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST) kwa kuwa taasisi ya kwanza ya Umma kufanya malipo ya mirabaha kwa ajili ya matumizi ya kazi za maandishi. Hii ni kuonesha kwamba wanathamini juhudi na jitihada za watunzi katika kuhakikisha wananufaika na kazi zao wanazozitunga. Aidha, maduka matatu ya kutoa fotokopi katika Mkoa wa Mjini Magharibi yamefanya malipo ya mirabaha.

**93. Mheshimiwa Spika,** katika kupunguza uharamia wa Hakimiliki, Afisi imefanya ukaguzi katika maeneo ya watumiaji na wamefanikiwa kukagua maeneo **112.** Maeneo yaliyokaguliwa ni maduka ya kuuza na kukodisha kazi za vinasa sauti vya kusikia na kuona **17,** Mahoteli 58, Kumbi za Burudani **5,** Vituo vya Utangazaji **7,** Vyombo vya Usafiri **4** na maduka ya fotokopi **21.** Watumiaji hao walielimishwa juu ya matumizi sahihi ya kazi za hakimiliki, kuepuka uharamia na umuhimu wa kulipia mirabaha ili waweze kufanya biashara zao kihalali. Aidha, vifaa vilivyokamatwa ambavyo vilitumika kufanyia uharamia vyenye uzito wa tani **2** vipo katika utaratibu wa kuangamizwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mazingira Zanzibar kwa kufuata taratibu za Sheria za Zanzibar.

**94. Mheshimiwa Spika,** katika kukuza vipaji vya wasanii, Wizara imefanikiwa kuandaa mashindano ya filamu fupi fupi zenye maudhui ya “Uchaguzi wa Amani” ambapo jumla ya filamu **5** za wasanii wa Zanzibar, zilishiriki katika

mashindano hayo. Kilele cha mashindano hayo kilifanyika Oktoba 16, 2020, ambapo washindi **3** kutoka vikundi tafauti waliibuka na ushindi na walikabidhiwa tunzo na zawadi mbali mbali. Washindi hao ni, Mshindi wa kwanza ni Nd. Salum Maulid Salum, Mshindi wa Pili ni kikundi cha Sanaa cha JKU na Mshindi wa tatu ni kikundi cha Sanaa cha KVZ. Lengo la mashindano hayo ni kuwajengea uwezo na kuweza kushindana katika soko la filamu la ndani na nje ya nchi.

**95. Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara kupitia Afisi ya Hakimiliki inapitia mkataba wa msanii wa muziki wa kizazi kipya ambae anatarajia kufunga mkataba huo na kampuni ya *Paradise Africa PTY LTD* ambayo inafanya kazi ya kuingiza na kuzionesha kazi za wasanii katika mitandao ya kijamii kama Instagram, *Facebook, Tiktok, Webchat,* Snapchat n.k. Vile vile wabunifu na wasanii wagonjwa **30** wamefikiwa katika maeneo yao kwa Unguja na Pemba. Aidha, mkutano wa wasanii umefanyika tarehe 22 Januari, 2021, na kusikiliza changamoto zinazowakabili wasanii katika utayarishaji wa kazi zao na kuzitafutia ufumbuzi.

**96. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha haki na maslahi ya wasanii yanaimarishwa kwa kuboresha mazingira ya kisheria, Afisi imefanikiwa kuainisha maeneo ya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki, namba **14** ya mwaka 2003, ili Sheria hiyo iweze kwenda na wakati uliopo ikiwemo kuingiza vipengele vya mikataba na makubaliano ya kimataifa ya hivi karibuni ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia. Aidha, mkutano na wadau wa Hakimiliki juu ya marekebisho ya Kanuni ya Utoaji Leseni za Hakimiliki kwa maonesho kwa Umma na Utangazaji za mwaka 2009, na marekebisho yake ya mwaka 2010 umefanyika Machi 10, 2021. Wadau walipata nafasi ya kutoa maoni yao juu ya marekebisho ya Kanuni hizo kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili, yaani kwa upande wa wamiliki wa hakimiliki na watumiaji wa hakimiliki kibiashara.

97. **Mheshimiwa Spika,** Vipindi **5** vya elimu juu ya masuala ya Hakimiliki vilirushwa hewani kupitia televisheni ya "Zanzibar Cable" na ZBC kwa lengo la kuwaelimisha watumiaji wa kazi za hakimiliki, wamiliki na jamii kwa jumla juu ya haki za wabunifu na wasanii pamoja na umuhimu wa kulipia Mirabaha kwa matumizi ya hakimiliki kwa lengo la kuinua kipato cha wabunifu na wasanii. Vile vile, mfanyakazi 1 anaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Mali za Ubunifu ***(Master in Intellectual Property – MIP)*** katika Chuo cha Tongji cha Shanghai China kwa njia ya mtandao hapa Zanzibar kutokana na kuendelea kwa janga la Korona huko China.

**Programu ndogo 2: Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo**

98. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo inatekelezwa na Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ). Kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 3,277,200,000/=** ambapo **shilingi 777,200,000/=** kwa kazi za kawaida na jumla ya **shilingi 2,500,000,000/=** kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. Hadi kufikia Machi 2021, **shilingi 1,296,195,010/=** sawa na asilimia **40** zimepatikana kati ya hizo **Shilingi 64,616,000/=** sawa na asilimia 8 ni matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya **Shilingi 1,231,579,010/=** sawa na asilimia **49** ni fedha za utekelezaji wa Mradi wa uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.
**(Angalia kiambatisho namba 1D)**

99. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programu hii kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ilipanga kuimarisha na kuendeleza vituo vya michezo kwa ajili ya kuibua vipaji; kusaidia timu za Taifa, vilabu na Vyama vya Michezo kushiriki na kuandaa mashindano ya kitaifa na kimataifa; kuandaa mashindano ya Mawizara, Mashirika na

Taasisi za Serikali. Aidha, Wizara imewasaidia viongozi wa vyama vya michezo, waamuzi na makocha kushiriki mafunzo ya kitaifa na kimataifa na kuimarisha uwanja wa Amaan, Gombani, Mao-Zedong na viwanja vya Wilaya.

100. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha vituo vya michezo na kuibua vipaji kwa vijana, Wizara inaendelea kuratibu mafunzo ya waamuzi wadogo wa mpira wa miguu ambapo jumla ya vijana **21** wanaendelea na mafunzo katika chuo cha Michezo cha JKU ***(JKU Academy)*** kilichopo Kama. Matumaini ya Wizara ni kupata waamuzi vijana wenye ubora katika Taifa letu.

101. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza michezo nchini Wizara kupitia Idara ya Michezo imefanikiwa kusaidia mafunzo ya Ukocha kwa chama cha mpira wa mikono Zanzibar (Handball) ambapo jumla ya washiriki **51** kati ya hao wanawake **10** na wanaume **41** walishiriki mafunzo ya awali yaliyofanyika huko Pemba. Aidha, jumla ya washiriki **50** ambapo washiriki **39** kutoka Unguja, **10** Tanzania Bara na 1 kutoka Pemba walishiriki mafunzo ya Kati. Mafunzo yote hayo yaliendeshwa na Mtaalamu kutoka Ujerumani Bwana MORITZ HERTHUM kupitia jumuia ya ***State Sport Association of Lower Saxon*** ya Ujerumani mwezi Agosti 2020. Vile vile, mafunzo ya waamuzi wa chama cha ***Handball*** yalitolewa ambapo jumla ya washiriki **21** wakiwemo wanawake **4** na wanaume **17** walishiriki mafunzo ya kati na Mtaalamu wa mafunzo hayo ni Bwana Charles Omondi kutoka nchini Nairobi – Kenya mwezi wa Disemba – Januari 2020/2021.

102. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yalifanyika Unguja na kufana sana. Jumla ya timu **9** zilishiriki katika mashindano hayo zikiwemo 5 kutoka Tanzania Bara, **2** Unguja na **2** Pemba. Kupitia mashindano hayo, Wizara iliweza kudhibiti mapato

na kuhakikisha kuwa Serikali haitoi pesa za kuendesha mashindano hayo na hivyo kuokoa pesa za Serikali. Vile vile, Wizara imeweza kudhibiti changamoto za migogoro kwenye michezo na sasa inaadaa utaratibu mzuri wa utawala bora michezoni.

103. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na chama cha Mazoezi ya viungo Zanzibar (ZABESA) imefanikisha kuandaa tamasha la siku ya mazoezi ya Viungo Kitaifa ambalo limefanyika katika Uwanja wa Amaan. Tamasha hilo limefanyika tarehe 1 Januari, 2021 jumla ya vikundi **97** vilishiriki, kati ya hivyo, vikundi **60** kutoka Unguja, vikundi **20** kutoka Pemba na vikundi **17** kutoka Tanzania Bara. Katika Tamasha hilo mgeni rasmi alikuwa ni **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.** Kauli mbiu ni ***"Kuimarisha Uchumi wa Buluu, afya bora kwanza".***

104. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Sera ya Michezo ya 2018, Wizara imefanikiwa kusimamia mashindano ya Mawizara na Mashirika ya Serikali ambayo yaliweza kusaidia sana katika kuleta hamasa ya michezo kwa watumishi wa umma kufuatia michezo mbalimbali kuchezwa katika kipindi hicho ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa mikono, mpira wa pete, mpira wa wavu, mpira wa kikapu, Riadha, Bao na Karata. Jumla ya timu zilizoshiriki ni **21** zikiwemo timu za Mawizara na Mashirika ya Serikali. Hali ambayo ilipelekea kuibua hamasa kwa wachezaji na kuimarisha mashirikiano, udugu na umoja miongoni mwa Mawizara pamoja na Taasisi kuanzisha Timu za Michezo mbali mbali.

105. **Mheshimiwa Spika,** vilabu viwili vya mchezo wa Riadha na Judo vimesaidiwa kuandaa na kushiriki mashindano ya Kimataifa. Aidha, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limekiwezesha chama cha Mchezo wa Judo kuandaa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ya

mchezo huo. Matokeo ya mashindao hayo ni Zanzibar kupata medali 13 za dhahabu na fedha. Katika mashindano hayo, Zanzibar ndio iliyokuwa wenyeji. Pia, Chama cha mchezo wa Riadha kimesaidiwa kushiriki mashindano ya ***Taifa Cup*** yaliyofanyika Dar es salaam.

**106. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar imeweza kukutana katika kuendeleza na kuimarisha mashirikiano na Taasisi zinazosimamia michezo kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Baraza limeweza kushiriki katika kikao cha pamoja kati ya BTMZ, BMT na vyama pacha vya michezo ya Riadha na JUDO. Kikao hicho kilifanyika Dar es Salaam. Lengo la kikao hicho ni kujadili uteuzi wa wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania watakaoshiriki mashindano ya Olimpiki yatakayofanyika mwaka 2021 Tokyo, Japan. Kwa upande wa Zanzibar, kijana mmoja amefikia kiwango kinachotakiwa na anatarajiwa kuiwakilisha Tanzania katika mashindano hayo.

**107. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza limeweza kufanikisha kufanyika Mkutano wa wadau wa michezo ambao ulipelekea kupatikana kwa wajumbe wanne (4) wa Baraza wanaowakilisha vyama vya michezo. Aidha, kupitia Mkutano huo, Baraza lilipokea maoni ya wadau kuhusiana na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar. Baraza limefanikiwa kukutana na viongozi wa vilabu vya michezo mbalimbali vilivyoko katika Wilaya zote za Pemba. Lengo la mkutano huo ni kutoa mafunzo kwa viongozi wa vilabu kuhusiana na ulipaji ada ya mwaka pamoja na kufanya uchaguzi.

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanya mikutano 4 na Vilabu vya Pemba ili kutatua mgogoro wa timu kugoma kucheza ligi ya daraja la Kwanza Taifa. Mkutano wa vilabu vyote ulifanyika Pemba ili kusikiliza changamoto na hatimae kuzipatia ufumbuzi. Matokeo ya mikutano hiyo ni kwamba mgomo Pemba umemaliza na ligi inaendelea kuchezwa.

**109. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imezitembelea baadhi ya Akademi na kufanya mazungumzo na viongozi na wazazi wa wachezaji. Akademi mbili za mpira wa miguu ziliiomba Wizara kuwaruhusu kutumia Uwanja wa Mao kwa ajili ya mazoezi na hivyo kuendeleza vipaji vya watoto. Ruhusa hiyo imetoka na sasa vijana wanafanya mazoezi kwa utaratibu uliowekwa.

**Mradi wa uimarishaji wa Viwanja vya Michezo**

**110. Mheshimiwa Spika,** mradi wa uimarishaji wa Viwanja vya Michezo unatekelezwa ndani ya programu ndogo ya uimarishaji na uendelezaji wa michezo, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mradi huu umepangiwa jumla ya **shilingi 2,500,000,000/=** hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 1,231,579,010/=** zimepatikana sawa na asilimia **49.**

**111. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulipangiwa shughuli za kuimarisha kiwanja cha Amaan na Gombani kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya umeme, uwekaji wa ubao wa matangazo (score board) katika kiwanja cha Gombani na uwekaji wa taa katika minara kwa viwanja vyote viwili hivyo.

**112. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika juhudi zake za kuimarisha viwanja vya michezo imefanikiwa kuimarisha miundombinu ya michezo kwa kukamilisha uwekaji wa nyasi bandia na ubao wa matangazo pamoja na uwekaji wa vipaza sauti ***(Public Adress System)*** umekamilika katika Uwanja wa Amaan. Aidha, taa za kisasa zinazotumia umeme mdogo zimeshanunuliwa na zitafungwa katika uwanja wa Amaan mara tu zitakapofika nchini mwezi wa Juni 2021.

**113. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza michezo Wizara imekamilisha ujenzi wa viwanja vya Wilaya kwa awamu ya

kwanza. Viwanja vyenyewe ni Kangani (Wilaya ya Mkoani) na Kishindeni (Wilaya ya Micheweni) kwa upande wa Pemba. Viwanja hivyo vimekabidhiwa kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na sasa vimeanza kutumika. Lengo kuu la kujengwa viwanja hivi ni kutumika katika shughuli mbali mbali pamoja na kuwapa fursa vijana kuvitumia ili kuweza kuibua vipaji na kuweza kukuza michezo nchini na kuleta umoja, amani na mshikamano miongoni mwa jamii kupitia mashindano mbalimbali ya michezo watakayoanzisha na hii ndio azma ya Serikali. Awamu ya pili ya ujenzi itajumuisha kutia uzio, kujenga vyoo na vyumba vya kubadilisha nguo.

114. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na ujenzi wa viwanja viwili vya Wilaya vilivyopo Unguja ambapo fedha zake zilitokana na bajeti ya 2018/2019 ambapo jumla ya **shilingi 800,000,000/=** ziliidhinishwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Jumla ya fedha zilizotoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni **shilingi 459,943,800/=** ambazo ziliingizwa Wizarani katikati ya mwaka, 2020 na kulipwa kwa Wakala wa Barabara Zanzibar kwa ujenzi wa viwanja viwili. Kiwanja kimoja kilichopo katika eneo la Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini "A" kinajengwa kwa gharama ya **shilingi 205,750,000/=**. Kiwanja cha pili kilichopo katika eneo la Kama Wilaya ya Magharibi "A" kimepangiwa kutumia kwa gharama ya **shilingi 254,193,800/=**.

115. **Mheshimiwa Spika,** viwanja hivyo vilivyojengwa kwa awamu ya kwanza ***(phase one)*** ambapo ni kusafishwa kwa eneo la kiwanja, kujaza fusi kwa ajili ya kupata level ya kiwanja kuwa sawa na kutandaza udongo kwa kuotesha majani kwa ajili ya eneo la kuchezea ***(pitch),*** kuweka lami katika eneo la kukimbilia ***(running track)*** na kujenga kiwanja cha michezo midogo midogo ***(4 in 1)*** ambayo inajumuisha michezo ya mpira wa mikono, mpira wa kikapu, mpira wa pete na mpira wa wavu.

116. **Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa kiwanja kilichopo Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja umeshafikia zaidi ya asilimia **80** ya ujenzi huo ambao upo katika hatua za mwisho baada ya mjenzi kutawanya kifusi kwenye eneo la kuchezea tayari akisubiria majani kuota. Mkandarasi anamalizia ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji pembezoni mwa kiwanja hicho. Vile vile katika kiwanja hicho kuna kiwanja cha michezo midogo midogo **(4 in 1)** chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo wa Serikali.

117. **Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa kiwanja cha Michezo kilichopo Kama Wilaya ya Magharibi 'A' umesitishwa kufuatia mapungufu yaliyojitokeza ikiwemo kutokuwepo kwa mkataba wa kuanza kazi, eneo liliopo kiwanja sio rafiki kwa ujenzi wa kiwanja na pia kitahitaji pesa nyingi sana kwa vile kimeinuka katika baadhi ya maeneo yake na fedha iliyopangwa ni kidogo ukilinganisha na ujenzi wa kiwanja hicho. Pia, kuna hatari ya kutokea mgogoro kwa muwekezaji wa Utalii katika utumiaji wa njia ilipo kati kati ya eneo lililotengwa kwa ajili ya mradi wa kiwanja.

**iii Programu ya Uendelezaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo.**

118. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,540,292,400/=** kati ya hizo **shilingi 1,390,561,900/=** ni mishahara na **shilingi 1,149,730,500/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **shilingi 707,258,607/=** sawa na asilimia **50** zilipatikana kati ya hizo **shilingi 603,806,155/=** ni mshahara na **shilingi 103,452,452/=** ni matumizi mengineyo.

**Programu ndogo 1: Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

119. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,473,725,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imefanikiwa kupata **shilingi 682,258,607/=** sawa na asilimia **46** ya fedha zilizopatikana **(angalia kiambatanisho namba 1D).**

120. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi, Wizara ilijipangia shughuli zifuatazo; kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi, kuandaa mpango wa manunuzi na mpango wa matumizi ya fedha.

121. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kutoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi juu ya utayarishaji wa mpango wa urithishwaji wa madaraka na uingizaji wa taarifa za watumishi katika mfumo wa kielektroniki (kanzi data). Mafunzo haya yalilenga kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu ya kila siku ya wafanyakazi.

122. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya mikutano kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa taasisi zake zote zilizopo Unguja na Pemba juu ya kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa Umma, sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Idara imeratibu Mikutano ya Kamati za Uongozi na Kamati Tendaji ya Wizara kwa lengo la kuongeza ufanisi na kasi kubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

123. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia ziara za kikazi kwa viongozi wakuu wa Wizara

katika Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa upande wa Pemba, Dar es Salaam pamoja na Taasisi zilizopo Dodoma zinazofanya kazi kwa mashirikiano na Wizara. Ziara hizo zimeweza kuimarisha ushirikiano na wadau wa Wizara pamoja na kusimamia kwa ukaribu utendaji wa kazi katika Taasisi hizo, kutafuta fursa mbalimbali za vijana pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili watendaji.

124. **Mheshimiwa Spika,** Idara katika kutekeleza majukumu yake kiutendaji ya kila siku, imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi kwa kuwapatia vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya kazi kwa ajili ya kuongeza bidii na kuimarisha ufanisi wa kazi. Pia wafanyakazi wote wamepatiwa stahiki zao kama vile malipo baada ya saa za kazi, fedha za likizo, haki ya mapumziko baada ya kujifungua mtoto. Aidha, Idara inaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano.

125. **Mheshimiwa Spika,** katika kuleta ufanisi mzuri wa matumizi ya rasilimali fedha, Idara imeweza kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ripoti za fedha kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma yanafanyika kwa usahihi. Pia, mafunzo kwa maafisa manunuzi na wahasibu yametolewa chini ya uwezeshaji kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

126. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imesimamia nidhamu kazini kwa kutembelea taasisi zake mbali mbali na kuwaonya wafanyakazi wanaochelewa. Uongozi wa Wizara ulifanya mkutano na wafanyakazi wa taasisi zake za Unguja na Pemba na kubadilishana nao mawazo, kitendo kilichowafurahisha wafanyakazi na kuomba tabia hiyo kuendelezwa. Ziara hii ilitoa funzo kwa Wizara nyengine.

**Programu Ndogo 2: kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.**

127. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

128. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2020/2021 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 170,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2021 imefanikwa kupata jumla ya **shilingi 25,000,000/=** sawa na asilimia **15** ya fedha zilizopatikana **(angalia kiambatanisho namba 1D).**

129. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka 2020/2021 shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa. Kufanya mapitio ya sera, kuandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu, kuandaa tafiti za Wizara, kuandaa bajeti ya Wizara na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi na programu za Wizara.

130. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kuipeleka kwa wadau wa lugha sera ya Lugha ya Kiswahili kwa Unguja na Pemba, ambapo wataalamu 82 wa Lugha ya Kiswahili kutoka katika Wizara zote za Serikali, taasisi za Serikali na taasisi binafsi walihudhuria katika kikao hicho kwa ajili ya kupata michango ya kuboresha rasimu ya sera hiyo.

131. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa taarifa za utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara na kuwasilisha inapohusika ikiwemo taarifa za utekelezaji wa bajeti, taarifa ya utekelezaji wa maagizo **13** ya **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025 pamoja na ripoti

za tathmini za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Idara imeandaa mpango wa mwaka wa utekelezaji na inaendelea na uandaaji wa mpango wa miaka mitano wa Wizara. Idara imeandaa hotuba ya bajeti kwa mwaka 2021/2022.

132. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanya ufuatiliaji na tathmini juu ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa upande wa Unguja na Pemba. Mradi iliotembelewa ni mradi wa ujenzi wa kiwanja cha Michezo kilichopo Mkokotoni Wilaya ya kaskazini 'A' na Miradi ya Vijana ya Green house na viwanja vya michezo vya Wilaya.

133. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya utafiti mdogo juu ya kuwatambua wachezaji wakongwe waliocheza katika miaka ya 1970 ambapo wachezaji 300 walifikiwa kwa upande wa Unguja na Pemba. Utafiti huo umegundua kuwa wachezaji hao hawashirikishwi ipasavyo katika kutoa michango yao.

Programu ndogo 3: Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba.

134. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 896,567,400/=**. Kwa kazi za kawaida jumla ys **Shilingi 299,730,500/=** na mishahara **shilingi 596,836,900/=** zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2021, imefanikiwa kupata jumla ya **shilingi 558,096,085/=** sawa na asilimia **62 (angalia kiambatanisho namba 1A).**

135. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa kuratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi wa Ofisi kuu Pemba; kutoa uelewa kwa wafanyakazi

kuhusiana na masuala mbalimbali katika kuimarisha utendaji kazi; kusimamia shughuli za miradi inayotekelezwa Pemba na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiutendaji za Wizara zinazofanyika Unguja na nje ya Zanzibar.

136. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji wa ofisi. Huduma zilizotolewa ni pamoja na ununuzi wa gari moja la ofisi, vifaa vya kuandikia, upatikanaji wa huduma za maji na umeme, malipo ya masomo ya muda mrefu kwa mfanyakazi 1 wa ngazi ya stashahada. Aidha, stahiki muhimu za wafanyakazi kama vile malipo ya safari kikazi kwa wafanyakazi 18, malipo ya likizo kwa wafanyakazi 8, malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi 16, na ubani wa kufiwa kwa wafanyakazi 2 zimetolewa.

137. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kuratibu Mikutano ya wafanyakazi Pemba ambapo jumla ya mikutano minne (4) imefanyika. Mikutano miwili kati ya hiyo ni ya kumtambulisha Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na kutoa nasaha zao na kusikiliza changamoto za wafanyakazi. Mkutano wa wadau wa Wizara uliowashirikisha vijana 56 umefanyika, ukiwa na lengo la kujadili mambo mbalimbali yanayohusu vijana. Aidha, kuratibu vikao na ziara za wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa jamii ya Baraza la Wawakilishi, zikiwemo kutembelea ujenzi wa studio za Shirika la Utangazaji Zanzibar, pamoja na kiwanja cha Kishindeni.

138. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya ziara sita (6) za ufuatiliaji na tathmini wa Miradi na shughuli za Ofisi zimefanyika, ikiwemo ziara ya Mheshimiwa Waziri ya kutembelea Miradi ya Programu ya Ajira kwa Vijana Pemba, ziara ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu ya kutembelea miradi ya Wizara kwa upande wa Pemba; ziara ya Ofisa mdhamini ya kutembelea na kukagua Miradi ya Programu ya Ajira kwa Vijana na kutembelea minara ya kurushia matangazo iliyoko

Kichunjuu na Bungala. Pia ziara ya kutembelea vikundi vya wajasiriamali vijana katika Wilaya 4 za Pemba ambapo jumla ya vikundi 28 vya vijana vimefikiwa; ziara ya kutembelea vikundi 16 vya sanaa na utamaduni na wasanii wakongwe Pemba na ziara ya ufuatiliaji na tathmini kwa vijana wa kike ambao wamepatiwa mafunzo ya uongozi ambapo jumla ya Vijana 140 walishiriki.

139. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imekusanya takwimu mbali mbali zinazohusu shughuli za kiuchumi za vijana, shughuli za michezo, sanaa na utamaduni. Jumla ya Shehia 68 za Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Chake Chake zilihusika. Takwimu hizi zitasaidia kutathmini hali za vijana na maendeleo ya michezo, sanaa na utamaduni yaliyofikiwa.

140. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zimetayarishwa na kuwasilishwa kunakohusika, zikiwemo Taarifa za utekelezaji wa mpango kazi, taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025, taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais na Taarifa ya mafanikio ya WHVUM ya miaka 10 (kuanzia 2010 hadi 2020) ya utawala wa Mhe. Rais mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein.

141. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi kuu Pemba imeratibu mafunzo ya siku 6 kwa Vikundi 6 vya Vijana ambapo kila kikundi kilipatiwa mafunzo hayo kwa siku 1. Mafunzo hayo yalilenga kuwaelimisha Vijana hao juu ya masuala ya ufugaji wa Kuku, uongozi na mgawanyo wa majukumu kwa wanachama wa vikundi, utunzaji wa Kumbukumbu, uandishi wa ripoti, uandishi wa kumbukumbu za vikao na kujitambua. Aidha, ziara ya ufuatiliaji na tathmini imefanyika kwa vikundi ambayo vimepatiwa mafunzo hayo ili kufahamu ni kwa kiasi gani wameyafanyia kazi mafunzo yao na wamenufaika vipi.

142. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imesimamia uchaguzi za mabaraza ya vijana ya Shehia **129** za Pemba. Uchaguzi umekamilika

katika hali ya usalama na amani na kila Shehia imechagua Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti, Katibu na Kamati Tendaji yenye wajumbe tisa. Lengo la kuundwa mabaraza haya ni kuwakutanisha vijana katika Shehia ili waweze kujadili mambo mbali mbali yanayowahusu yakiwemo ya kijamii, ya kisiasa na kiuchumi na uzalendo. Pia kuwawezesha vijana kujitambua na hukuza mahusiano ya vijana ndani na nje ya nchi.

## F. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

143. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na kueleza utekelezaji na mafanikio ya Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imepangiwa jumla ya **shilingi 70,893,081,000/=**. Kati ya fedha hizo **shilingi 14,424,100,000/=** kwa matumizi ya kawaida na **shilingi 56,468,981,000/=** kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

144. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za matumizi ya kazi za kawaida jumla ya **shilingi 8,299,500,000/=** ni kwa ajili ya mishahara ambapo **shilingi 3,861,800,000/=** ni mishahara ya Idara za ndani ya Wizara na **shilingi 4,437,700,000/=** ni mishahara kwa taasisi nyengine zinazopokea ruzuku. Kwa upande wa matumizi mengineyo jumla ya **shilingi 6,124,600,000/=** kati ya hizo matumizi mengineyo kwa Idara za Wizara ni jumla ya **shilingi 2,154,000,000/=** na kwa taasisi zinazopokea ruzuku ni jumla ya **shilingi 3,970,600,000/=**.

145. **Mheshimiwa Spika,** katika fedha za miradi ya maendeleo, Wizara imepangiwa jumla ya **shilingi 56,468,981,000/=** ikiwa ni mchango kutoka Serikalini kama ifuatavyo:

i. Programu ya Ajira kwa Vijana **Shilingi 7,000,000,000/=**;
ii. Programu ya uimarishaji na utoaji wa Matangazo (ZBC) **shilingi 19,201,500,000/=**;

iii. Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya **shilingi 4,000,000,000/=**;
iv. Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya nje na Academy **shilingi 3,000,000,000/=**;
v. Mradi wa Ununuzi wa Mtambo mwengine wa Kuchapia Magazeti **shilingi 13,747,481,000/=**; na
vi. Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa inayoendana na Teknolojia za Kisasa za Uchapaji **shilingi 9,520,000,000/=**.

**146. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 1,384,226,000/=** kutoka vyanzo mbali mbali kupitia taasisi zake.

## G. MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022

**147. Mheshimiwa Spika,** Wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo :-
i. Kuimarisha miundombinu ya Habari kwa ajili ya uzalishaji na urushwaji wa vipindi, ununuzi wa maudhui, ufuatiliaji wa habari, ununuzi wa mitambo ya uchapaji. Pia itaendelea na uchapishaji na usambazaji wa magazeti ili jamii iweze kupata taarifa sahihi na kwa wakati.;
ii. Kuimarisha huduma za maendeleo ya Vijana kwa kuanzisha mfuko wa Mikopo kwa vijana na kuanzisha vituo cha Vijana;
iii. Kuimarisha huduma za utamaduni kwa kujenga Chuo cha Utamaduni na kuandaa mpango wa Kiswahili na kufuatilia fursa zilizopo za mahitaji ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza ajira na kukuza, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, Sanaa na ubunifu kwa jamii ya Zanzibar ili haki na maslahi ya wasanii na wabunifu zipatikane;

iv. Kuimarisha miundombinu ya michezo pamoja na kuviwezesha vyama vya michezo kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sera, Sheria ya Baraza na kanuni za mashirikisho ya michezo ya kimataifa, kikanda na Kitaifa na kuzisadia timu za Taifa na za watu wenye ulemavu; na
v. Kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi na wafanyakazi ikiwemo utoaji wa vitendea kazi na stahiki za wafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kuwaendeleza kwa kuwapatia mafunzo.

## H. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**148. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo itatumia jumla ya **shilingi 70,893,081,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu nne ambazo ni:-

i. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji **(shilingi 50,119,606,000/=)**;
ii. Programu ya Maendeleo ya Vijana **(shilingi 7,538,121,000/=)**;
iii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo **(shilingi 10,473,618,000/=)**; na
iv. Programu ya Utawala, Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. **(shilingi 2,761,736,000/=)**.

**(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F, 1G na 1H)**.

**Programu Kuu PJ0301: Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji (shilingi 50,119,606,000/=)**

**149. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongezeka kwa upatikanaji na usambazaji wa habari za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi kwa wananchi kwa wakati.

Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuona kuwa wananchi wanapata huduma na kutumia habari zenye kiwango bora. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 50,119,606,000/=** na imepangiwa kusimamia programu ndogo mbili:-

**i. Programu Ndogo SJ030101: Upatikanaji na Usambazaji wa Habari (shilingi 39,071,646,000/=)**

**150.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya upatikanaji na Usambazaji wa habari inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo: Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar, Shirika la Magazeti na Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui. Programu ndogo hii ina jukumu la kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ndogo ni utoaji wa taarifa kwa umma, usambazaji wa maudhui ya utangazaji na urushaji wa vipindi na matangazo kupitia TV na Redio na kuchapisha magazeti. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 39,071,646,000/=** ambapo **shilingi 13,747,481,000/=** kwa utekelezaji wa Mradi wa Ununuzi wa Mitambo Kuchapisha Magazeti uliopendekezwa kuwepo katika Wakala wa Uchapaji wa Serikali; **shilingi 19,201,500,000/=** kwa utekelezaji wa Programu ya Uimarishaji na Utoaji wa matangazo (ZBC) na **shilingi 6,122,665,000/=** kwa kazi za kawaida.

**ii. Programu Ndogo SJ030102: Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji (shilingi 11,047,960,000/=)**

**151.** **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ndogo ni kuwa na vyombo vya habari vinavyozingatia Sheria, kanuni na maadili ya habari. Matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuwa na usimamizi bora wa vyombo vya habari pamoja na upatikanaji wa habari zenye maadili. Programu hii

imepangiwa jumla ya **Shilingi 11,047,960,000/=** ambapo **shilingi 9,520,000,000/=** kwa utekelezaji wa Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya kisasa inayoendana na Teknolojia za Kisasa za Uchapaji na **shilingi 1,527,960,000/=** Kwa kazi za kawaida.

**152. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hizi shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kuimarisha uendeshaji wa Mashirika yaliyomo ndani ya Wizara kwa kununua mitambo mipya na ya Kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa huduma;
2. Kuboresha huduma ya upatikanaji na usambazaji taarifa na maudhui ya utangazaji kuwa ya kisasa ili kuwafikia wananchi wote wa Zanzibar;
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mashirika na kampuni zilizomo ndani ya Wizara kwa kuwapatia mafunzo ili kuendana na kasi Teknolojia inayokuwa kwa haraka duniani na kuleta ufanisi katika kazi zao; na
4. Kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanya kazi kwa kuwapatia vifaa vya kisasa na vinavyoendana na wakati.

**153. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hizi ziweza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 50,119,606,000/=** ambapo **shilingi 7,650,625,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 42,468,981,000/=** kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pia, makusanyo ya **shilingi 740,000,000/=** ambazo zinategemewa kukusanywa na Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji, Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP), Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji maudhui Zanzibar (ZMUX), Shirika la Utangazaji (ZBC) na Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS).

**Programu Kuu PJ0302: Maendeleo ya Vijana (shilingi 7,538,121,000/=).**

**154. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii, ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana ikiwa ni pamoja na kuwawezesha vijana ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia programu mbali mbali. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuongeza idadi ya ajira kwa vijana kwa kuwawezesha ikiwemo kuwajengea uwezo kupitia programu mbali mbali. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 7,538,121,000/=**.

**i. Programu Ndogo SJ030201: Maendeleo ya Vijana (shilingi 7,538,121,000/=)**.

**155. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana Zanzibar. Jukumu la msingi katika Programu ndogo ni kuwawezesha Vijana ili kujenga uzalendo, kupanua demokrasia, kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli za Maendeleo ya Vijana, kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru wa Kitaifa, kusimamia uendeshaji wa Mabaraza ya Vijana katika ngazi zote, kuyawezesha Mabaraza ya Vijana kiuchumi ili yaendeleze ajira kwa Vijana.

**156. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kuwaendeleza vijana kwa kuweka mazingira mazuri ikiwemo kutoa elimu, kuwaunganisha na taasisi ili kupatia mikopo nafuu na kuwasaidia kutafuta masoko, kuwaunganisha Vijana kupata fursa za kifedha, masoko na mafunzo kwenye shughuli za Kilimo, Uvuvi, Biashara, Elimu ya stadi za maisha na Amali, ujasiriamali ili kuwawezesha kiuchumi, kijamii na kisiasa;

2. Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru Kitaifa pamoja na kuwapatia vijana elimu ya uzalendo kwa lengo la kuipenda nchi yao;
3. Kuyawezesha Mabaraza ya Vijana ya Wilaya kwa kuyapatia mafunzo ya uongozi, kuwa na ofisi, samani za ofisi, Wafanyakazi pamoja na kuwaunganisha vijana katika fursa mbali mbali za kijamii na kiuchumi;
4. Kuendelea kuyaimarisha Mabaraza ya Vijana kwa kufanya mikutano yao kwa mujibu wa Sheria; na
5. Kuimarisha upatikanaji wa huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wa Taasisi zinazotekeleza programu hii.
6. Kuanzisha kituo cha Vijana (Youth Incubation Centre) kitakachosaidia vijana kupata huduma mbali.

157. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 7,538,121,000/=** ambapo **Shilingi 538,121,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 7,000,000,000/=** kwa utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana.

**Programu Kuu PJ0303: Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (Shilingi 10,473,618,000/=)**.

158. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa utamaduni, Lugha ya Kiswahili na Sanaa ya Zanzibar inawaendeleza wasanii kiuchumi ili kupunguza umasikini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni na kukuza michezo kwa kuwa na miundombinu yenye viwango vya kimataifa na kupata medali katika mashindano mbali mbali ya michezo na kuimarisha afya za wananchi, umoja na mshikamano nchini. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 10,473,618,000/=** na itakuwa na programu ndogo moja.

i. Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo **(shilingi shilingi 10,473,618,000/= )**.

**i. Programu Ndogo SJ030301: Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (shilingi shilingi 10,473,618,000/= )**.

**159. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya maendeleo ya utamaduni, sanaa na michezo inatekelezwa na Idara ya Utamaduni, Idara ya Michezo, Baraza la Michezo, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Jukumu la msingi katika programu ndogo ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za utamaduni, sanaa, haki za wasanii na michezo Zanzibar.

**160. Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za sanaa na wasanii, kujenga chuo cha sanaa, kurikodi kazi za sanaa kupitia studio ya filamu na muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili, usimamizi wa hakimiliki pamoja na ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wenye hakimiliki, uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo.

**161. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu ndogo hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kusimamia, kuhamasisha, kukuza, kuendeleza pamoja na kutoa elimu kuhusiana na matumizi bora ya lugha ya Kiswahili na lahaja zilizopo ndani na nje ya nchi;
2. Kuimarisha, kuvijengea uwezo vikundi vya sanaa vya Taifa pamoja na kuvisaidia vikundi vya Sanaa vya Wilaya na Shehia;
3. Kusajili, kusimamia, kukagua pamoja na kudhibiti kazi

na haki za wasanii na wabunifu wa kazi za sanaa pamoja na kuwapatia mirabaha yao;

4. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa taasisi zinazotekeleza programu ndogo hii;
5. Kuendeleza michezo kwa kuziwezesha timu kushiriki na kuandaa mashindano ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuvisaidia vyama vya michezo;
6. Kuimarisha, kuitunza na kuendeleza miundombinu ya michezo kwa kuviwekea mazingira bora Kiwanja cha Amani, Gombani, Mao- Zedong na viwanja vya Wilaya pamoja na kuandaa bonanza ya siku ya mazoezi ya viungo;
7. Kuandaa mafunzo ya Kitaifa na Kimataifa kwa waamuzi, makocha, viongozi na wanamichezo; na
8. Kuimarisha huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa taasisi zinazotekeleza programu ndogo hii; na
9. Kujenga miundombinu ya michezo ikiwemo Bwawa la kuogelea (swiming pool) la kisasa lenye viwango vya Kimataifa.

**162. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 10,473,618,000/=** kati ya fedha hizo **shilingi 3,473,618,000/=** kwa kazi za kawaida, **shilingi 7,000,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ya viwanja vya Wilaya, Bwawa la kuongelea na viwanja vya (**4** in **1**) na **shilingi 314,200,000/=** ni makusanyo ya fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Programu Kuu PJ0304: Utawala, Uendeshaji na Mipango katika sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (shilingi 2,761,735,000/=)**.

**163. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na utafiti pamoja na kuratibu na kusimamia utawala na uendeshaji mzuri wa

rasilimali watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa usimamizi bora wa mipango na uendeshaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 2,761,735,000/=** na itasimamia programu ndogo tatu.

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. **(shilingi 155,600,000/=)**;
ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo **(shilingi 1,683,026,000/=)**; na
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. **(shilingi 923,110,000/=)**.

**i. Programu Ndogo SJ030401: Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara (shilingi 155,600,000/=)**.

**164. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya Wizara.

**165. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo ni kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuratibu na kuandaa bajeti ya Wizara na kuratibu mipango na miradi ya maendeleo.

**166. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu ndogo hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Habari, Sera ya Utangazaji Zanzibar na kukamilisha Sera ya Lugha, Sera ya Filamu;
2. Kuratibu na kusimamia na kufanya tafiti za Wizara katika maeneo ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.;
3. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya michezo vya Wilaya, Mradi wa Ununuzi wa Mtambo wa kuchapia Magazeti, Mradi wa Ununuzi wa Mitambo mipya ya Kisasa inayoendana

na Teknolojia za Kisasa za Uchapaji, Programu ya Uimarishaji wa utoaji wa Matangazo (ZBC) na Programu ya Ajira kwa Vijana;

4. Kuandaa Bajeti, mipango ya muda mfupi na mrefu ya Wizara pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi, programu na shughuli za Wizara;
5. Kuimarisha upatikanaji wa huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa Taasisi zinazotekeleza programu ndogo hii; na
6. Kuendelea kuratibu vikao vya mashirikiano vya SMT na SMZ kwa Wizara na Taasisi zilizomo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**167. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 155,600,000/=** kwa kazi za kawaida.

**ii. Programu Ndogo SJ030402: Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (shilingi 1,683,025,000/=)**.

**168. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo itatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za Utumishi na Uendeshaji wa Wizara.

**169. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi.

**170. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu ndogo hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia vifaa, huduma muhimu pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao;
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa mujibu wa kada zao ili kufanya kazi kwa ufanisi pamoja na kufanya upimaji kwa wafanyakazi hao kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi zao;
3. Kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya masuala mtambuka ikiwemo udhalilishaji, Ukimwi, na mikakati ya kupambana na rushwa Zanzibar;
4. Kuratibu shughuli na ziara za kikazi za viongozi Kitaifa na Kimataifa;
5. Kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya mkakati wa kupambana na rushwa Zanzibar; na
6. Kuandaa na kusimamia mpango wa manunuzi wa Wizara.

**171. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,683,026,000/**= kwa kazi za kawaida.

**iii. Programu Ndogo SJ030403: Uratibu wa Shughuli za Wizara Afisi Kuu Pemba (shilingi 923,110,000/=)**.

**172. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Pemba. Programu ndogo hii ina jukumu la kuhakikisha mipango, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

**173. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo ni kusimamia na kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu Pemba. Huduma

ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera, utafiti na mipango mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba; kuratibu miradi ya maendeleo na kuwajenga uwezo wafanyakazi na mazingira bora.

**174. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu ndogo hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia vifaa, huduma muhimu pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa Ofisi Kuu Pemba;
2. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi na shughuli zote zinazotekelezwa Pemba;
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na kuendelea kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya Masuala ya uwajibikaji na uzalendo katika kazi; na
4. Kuwapatia mafunzo viongozi wakuu wa Idara za Pemba kuhusu Sera, utafiti na Mipango mikuu ya Wizara.

**175. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 923,110,000/=** kwa kazi za kawaida.

## I. SHUKRANI

**176. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kumaliza hotuba yangu mara nyengine tena naomba kuchukua fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitano (2020/2025) na kuanza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kasi kubwa.

177. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu kwa Katibu Mkuu Ndugu. Fatma Hamad Rajab, Naibu Katibu Mkuu Ndugu. Khamis Abdulla Said, Afisa Mdhamini Pemba, Makatibu Watendaji, Wakurugenzi, Kaimu Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi wa Wizara na wasaidizi wao pamoja na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa juhudi zao, uchapaji kazi, weledi wa maarifa, uadilifu na umakini mkubwa katika kazi zao.

178. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru waandishi wa habari wote, vijana wote, wanamichezo, wasanii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za Wizara yangu. Pia shukurani za pekee ziende kwa Vyombo vya Habari vya Serikali na Binafsi kwa kufanikisha kurusha vipindi mbali mbali vya kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Vijana, Utamaduni na taarifa za michezo.

179. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuzishukuru Wizara zote za Serikali pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali kwa mashirikiano mazuri wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji mzuri wa mipango ya Wizara. Vile vile, ninaishukuru Wizara ya Fedha na Mipango katika kuhakikisha kuwa fedha za maendeleo ya miradi na matumizi ya kawaida zinapatikana kwa wakati.

180. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika ya kimaendeleo ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Komoro, Afrika ya Kusini, Uganda, Ubalozi mdogo wa India, Ubalozi mdogo wa Oman, Shirika la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), UNDP, UNICEF, UNESCO, Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni (*World Intellectual Property Organisation* – WIPO), CRDB, NMB, Equity Bank, NIC, AZAM Media, Washirika wote wa Maendeleo tulioshirikiana nao katika utekelezaji wa

majukumu ya Wizara. Pia nawashukuru sana Waandishi wa habari na vyombo vyao kwa ushirikiano waliotupa.

181. **Mheshimiwa Spika,** naomba kukushukuru tena wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini mkubwa. Ni ukweli usiopingika kwamba mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii yamewezekana kutokana na ushirikiano wenu makubwa kabisa.

## J: MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

182. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya **shilingi 70,893,081,000/=**. Kati ya hizo **shilingi 6,124,600,000/=** ni kwa ajili ya kazi za kawaida, **shilingi 8,299,500,000/=** ni mishahara na **shilingi 56,468,981,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Pia, **shilingi 1,384,226,000/=** kwa makusanyo ya Wizara.

183. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima nawaomba wajumbe wako wa Baraza lako Tukufu waipitie, waijadili, washauri, watuelekeze na baadae waipitishe bajeti hii ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja

**Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita (MBM),**
**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**
**Zanzibar.**

# VIAMBATANISHO

KIAMBATISHO NAMBA 1 A

**FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| NO | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULY -MARCH 2020/2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 596,836,900 | 438,040,685 | 73% |
| | | Matumizi Mengineo | 299,730,500 | 120,055,400 | 40% |
| | **JUMLA** | | **896,567,400** | **558,096,085** | **62%** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 170,000,000 | 25,000,000 | 15% |
| | **JUMLA** | | **170,000,000** | **25,000,000** | **15%** |
| 3 | Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 793,725,000 | 603,806,155 | 76% |
| | | Matumizi Mengineo | 680,000,000 | 78,452,452 | 12% |
| | **JUMLA** | | **1,473,725,000** | **682,258,607** | **46%** |
| 4 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 148,915,000 | 111,883,020 | 75% |
| | | Matumizi Mengineo | 155,000,000 | 25,000,000 | 16% |
| | **JUMLA** | | **303,915,000** | **136,883,020** | **45%** |
| 5 | Idara ya Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 1,355,948,000 | 1,233,296,185 | 91% |
| | | Matumizi Mengineo | 300,000,000 | 65,750,000 | 22% |
| | **JUMLA** | | **1,655,948,000** | **1,299,046,185** | **78%** |
| 6 | Idara ya Michezo | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 630,000,000 | 37,000,000 | 6% |
| | **JUMLA** | | **630,000,000** | **37,000,000** | **6%** |
| 7 | Idara ya Habari Maelezo | Mishahara | 357,278,820 | 286,689,295 | 80% |
| | | Matumizi Mengineo | 384,183,450 | 188,209,112 | 49% |
| | **JUMLA** | | **741,462,270** | **474,898,407** | **64%** |
| | **Jumla ya Mishahara** | | **3,252,703,720** | **2,673,715,340** | **82%** |
| | **Jumla ya Matumizi Mengine** | | **2,618,913,950** | **539,466,964** | **21%** |
| | **Jumla Kuu kwa Taasisi zisizopokea Ruzuku** | | **5,871,617,670** | **3,213,182,304** | **55%** |

| | TAASISI ZA RUZUKU | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Vijana Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 217,200,000 | 64,790,000 | 30% |
| | | | **217,200,000** | **64,790,000** | **30%** |
| 2 | Afisi ya Msajili na Hakimiliki | Mishahara | 222,800,000 | 155,762,725 | 70% |
| | | Matumizi Mengineo | 366,800,000 | 63,944,000 | 17% |
| | **JUMLA** | | **589,600,000** | **219,706,725** | **37%** |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 216,000,000 | 66,988,000 | 31% |
| | **JUMLA** | | **216,000,000** | **66,988,000** | **31%** |
| 4 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 148,400,000 | 32,681,000 | 22% |
| | **JUMLA** | | **148,400,000** | **32,681,000** | **22%** |
| 5 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 147,200,000 | 27,616,000 | 19% |
| | **JUMLA** | | **147,200,000** | **27,616,000** | **19%** |
| 6 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 176,000,000 | 175,621,270 | 100% |
| | | Matumizi Mengineo | 199,000,000 | 76,978,896 | 39% |
| | **JUMLA** | | **375,000,000** | **252,600,166** | **67%** |
| 7 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 2,173,100,000 | 1,745,713,590 | 80% |
| | | Matumizi Mengineo | 1,872,400,000 | 276,594,199 | 15% |
| | **JUMLA** | | **4,045,500,000** | **2,022,307,789** | **50%** |
| 8 | Shirika la Magazeti | Mishahara | 416,000,000 | 399,629,410 | 96% |
| | | Matumizi Mengineo | 205,000,000 | 55,100,666 | 27% |
| | **JUMLA** | | **621,000,000** | **454,730,076** | **73%** |
| 9 | kampuni ya Uunganisha Maudhui (ZMUX) | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 357,800,000 | 79,078,230 | 22% |
| | **JUMLA** | | **357,800,000** | **79,078,230** | **22%** |
| | | | | | |
| 10 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | Mishahara | 917,300,000 | 649,893,440 | 71% |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ZGP) | Matumizi Mengineo | - | - | - |
| | **JUMLA** | | **917,300,000** | **649,893,440** | **71%** |
| | **Jumla ya Mishahara ya Ruzuku** | | **3,905,200,000** | **3,126,620,435** | **80%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya ruzuku** | | **3,729,800,000** | **743,770,991** | **20%** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **7,635,000,000** | **3,870,391,426** | **51%** |
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **7,157,903,720** | **5,800,335,775** | **81%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **6,348,713,950** | **1,283,237,955** | **20%** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA MATUMIZI YA KAWAIDA (A)** | | **13,506,617,670** | **7,083,573,730** | **52%** |
| | **Miradi ya Maendeleo** | | | | |
| 1 | Maendeleo ya Vijana. | | 2,000,000,000 | 600,000,000 | 30% |
| 2 | Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. | | 2,500,000,000 | 1,231,579,010 | 49% |
| 2 | Ununuzi wa Vifaa vya jingo la studio ZBC | | 1,400,000,000 | - | 0% |
| | **Jumla Kuu ya Wizara Miradi ya Maendeleo (B)** | | **5,900,000,000** | **1,831,579,010** | **31%** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)** | | **19,406,617,670** | **8,915,152,740** | **46%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1B**
**MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021**
**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 224,141,000 | 140,275,000 | 63% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 4,000,000 | 4,269,000 | 107% |
| 3 | Habari Maelezo | 69,111,000 | 78,734,250 | 114% |
| 4 | Tume ya Utangazaji | 314,142,375 | 170,370,560 | 54% |
| | **JUMLA** | **611,394,375** | **393,648,810** | **64%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1C**
**MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 150,000,000 | 87,562,289 | **58%** |
| **2** | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 1,000,000,000 | 596,891,493 | **60%** |
| **3** | Shirika la Magazeti | 857,500,000 | 592,990,940 | **69%** |
| **4** | ZAGPA | 9,614,628,000 | 2,880,754,708 | **30%** |
| **5** | ZMUX | 1,000,000,000 | 958,548,262 | **96%** |
| | **JUMLA** | **12,622,128,000** | **5,116,747,692** | **41%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1D**
**FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ya Maendeleo ya Vijana**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo ya Vijana | 303,915,000 | 136,883,020 | 45% |
| 2 | Baraza la Vijana Zanzibar | 217,200,000 | 64,790,000 | 30% |
| 3 | Programu ya Ajira kwa Vijana | 2,000,000,000 | 600,000,000 | 30% |
| | **JUMLA** | **2,521,115,000** | **801,673,020** | **32%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Idara ya Utamaduni na Sanaa | 1,655,948,000 | 1,299,046,185 | 78% |
| **2** | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 148,400,000 | 32,681,000 | 22% |
| **3** | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 216,000,000 | 66,988,000 | 31% |
| 4 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 589,600,000 | 219,706,725 | 37% |
| | **JUMLA** | **2,609,948,000** | **1,618,421,910** | **62%** |

**Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 630,000,000 | 37,000,000 | 6% |
| 2 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | 147,200,000 | 27,616,000 | 19% |
| 3 | Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo | 2,500,000,000 | 1,231,579,010 | 49% |
| | **JUMLA** | **3,277,200,000** | **1,296,195,010** | **40%** |

**Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,473,725,000 | 682,258,607 | 46% |
| | **JUMLA** | **1,473,725,000** | **682,258,607** | **46%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 170,000,000 | 25,000,000 | 15% |
| | **JUMLA** | **170,000,000** | **25,000,000** | **15%** |

**Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 741,462,270 | 474,898,407 | 64% |
| 2 | Shirika la Utangazaji ZBC | 4,045,500,000 | 2,022,307,789 | 50% |
| 3 | Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX) | 357,800,000 | 79,078,230 | 22% |
| 4 | Shirika la Magazeti ya Serikali | 621,000,000 | 454,730,076 | 73% |
| | **JUMLA** | **5,765,762,270** | **3,031,014,502** | **53%** |

**Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tume ya Utangazaji | 375,000,000 | 252,600,166 | 67% |
| 2 | Idara ya Habari Maelezo | 741,462,270 | 474,898,407 | 64% |
| 3 | Wakala ya SMZ wa Uchapaji (ZGP) | 917,300,000 | 649,893,440 | 71% |
| | **JUMLA** | **2,033,762,270** | **1,377,392,013** | **68%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 896,667,400 | 588,096,085 | 66% |
| | **JUMLA** | **896,667,400** | **588,096,085** | **66%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1E**
**FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**
**Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 224,141,000 | 140,275,000 | 63% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 4,000,000 | 4,269,000 | 107% |
| 3 | Habari Maelezo | 69,111,000 | 78,734,250 | 114% |
| 4 | Tume ya Utangazaji | 314,142,375 | 170,370,560 | 54% |
| 5 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 150,000,000 | 87,562,289 | 58% |
| 6 | Shirika la Magazeti | 857,500,000 | 592,990,940 | 69% |
| 7 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 1,000,000,000 | 596,891,493 | 60% |
| 8 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP) | 9,614,628,000 | 2,880,754,708 | 30% |
| 9 | Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) | 1,000,000,000 | 958,548,262 | 96% |
| | **JUMLA** | **13,233,522,375** | **9,243,698,275** | **69%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1F**
**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNINA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**
**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| No | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 673,110,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 250,000,000 |
| **JUMLA** | | | **923,110,000** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 155,600,000 |
| **JUMLA** | | | **155,600,000** |
| 3 | Uendeshaji na utumishi | Mishahara | 1,053,025,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 630,000,000 |
| **JUMLA** | | | **1,683,025,000** |
| 4 | Habari Maelezo | Mishahara | 328,225,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 359,740,000 |
| **JUMLA** | | | **687,965,000** |
| 5 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 158,421,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 140,900,000 |
| **JUMLA** | | | **299,321,000** |
| 6 | Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 1,649,018,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 317,760,000 |
| **JUMLA** | | | **1,966,778,000** |
| 7 | Michezo | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 300,000,000 |
| **JUMLA** | | | **300,000,000** |
| **Jumla ya Mishahara** | | | **3,861,800,000** |
| **Jumla ya Matumizi mengine** | | | **2,154,000,000** |
| **Jumla Kuu kwa taasisi zisizopokea Ruzuku** | | | **6,015,800,000** |

**TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Magazeti ya Serikali | Mishahara | 543,400,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 112,300,000 |
| | | | **655,700,000** |
| 2 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 2,326,700,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 2,058,900,000 |
| | | | **4,385,600,000** |
| 3 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | Mishahara | 1,104,100,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **1,104,100,000** |
| 4 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 250,800,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 152,800,000 |
| | | | **403,600,000** |
| 5 | Kampuni ya Unganishaji Maudhui (ZMUX) | Mishahara | **-** |
| | | Matumizi Mengineo | 393,400,000 |
| | | | **393,400,000** |
| 6 | Baraza la Vijana | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 238,800,000 |
| | **JUMLA** | | **238,800,000** |
| 7 | Afisi ya Msajili Hakimiliki | Mishahara | 212,700,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 403,300,000 |
| | **JUMLA** | | **616,000,000** |
| 8 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | 248,992,000 |
| | **JUMLA** | | **248,992,000** |
| 9 | Baraza la Sanaa,Sensa ya filamu na Utamaduni | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 200,208,000 |
| | **JUMLA** | | **200,208,000** |
| 10 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 161,900,000 |
| | **JUMLA** | | **161,900,000** |
| | **Jumla ya Mishahara Ruzuku** | | **4,437,700,000** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ruzuku** | | **3,970,600,000** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **8,408,300,000** |
| | | | |
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **8,299,500,000** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **6,124,600,000** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (Matumizi ya kawaida) A** | | **14,424,100,000** |

**MIRADI YA MAENDELEO**

| | **Miradi ya Maendeleo** | **Jumla ya fedha** |
|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Maendeleo ya Vijana | 7,000,000,000 |
| 2 | Uimarishaji wa viwanja vya Wilaya SMZ | 4,000,000,000 |
| 3 | Ujenzi WA Viwanja vya Nje na Academy | 3,000,000,000 |
| 4 | Programu ya Uimarishaji Utowaji Matangazo | 19,201,500,000 |
| 5 | Ununuzi wa Mtambo wa Kuchapia Magazeti | 13,747,481,000 |
| 6 | Ununuzi wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji | 9,520,000,000 |
| | **Jumla ya miradi ya maendeleo B** | **56,468,981,000** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA ( A + B)** | **70,893,081,000** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1G**

**BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo Vijana | 299,321,000 |
| 2 | Baraza la Vijana Zanzibar | 238,800,000 |
| 3 | Programu ya Ajira kwa Vijana | 7,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **7,538,121,000** |

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni na Sanaa na Michezo | 1,966,778,000 |
| 2 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 200,208,000 |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 248,992,000 |
| 4 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 616,000,000 |
| | **JUMLA** | **3,031,978,000** |

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 300,000,000 |
| 2 | Baraza la Michezo | 161,900,000 |
| 3 | Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja na Ujenzi wa Academy | 7,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **7,441,640,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 155,600,000 |
| | **JUMLA** | **155,600,000** |

**Programu Ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,683,025,000 |
| | **JUMLA** | **1,683,035,000** |

**Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji Zanzibar | 23,587,100,000 |
| 2 | Idara ya Habari Maelezo | 687,965,000 |
| 3 | Shirika la Magazeti | 14,403,181,000 |
| 5 | Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) | 393,400,000 |
| | **JUMLA** | **39,071,646,000** |

**Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Tume ya Utangazaji | 403,600,000 |
| 2 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 10,624,100,000 |
| | **JUMLA** | **11,047,960,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 MATUMIZI |
|---|---|---|
| | Ofisi Kuu Pemba | 923,110,000 |
| | **JUMLA** | **923,110,000** |

**KIAMBATISHI NAMBA 1H**
**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**
**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 300,000,000 |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 14,200,000 |
| 3 | Habari Maelezo | 300,000,000 |
| 4 | Tume ya Utangazaji | 440,000,000 |
| 5 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 250,026,000 |
| 6 | Ofisi Kuu Pemba | 80,000,000 |
| | **JUMLA** | **1,384,226,000** |